


MFUNGWA

 . . . hapa tena, katika Jina la Bwana Yesu, na kusikia juu ya kazi nyingi na kubwa ambazo Wewe umefanya, hapo kabla. Nasi sasa tunasimama kwa matarajio, uinue imani yetu na kututia mafuta, kuamini ya kwamba yale yaliyoombwa usiku wa leo yatakirimiwa. Wewe unajua kila moja ya hayo, yote ambayo wameomba. Nasi tunawaomba, hasa sana, Bwana, wale walio karibu na kufa. Lete amani kwa nafsi zao endapo tayari haipo. Lete oponyaji miilini mwao. Tujalie, Bwana.

² Bariki kukusanyika kwetu. Tu—tunaomba, Bwana, katika mkutano huu wa Jumatano usiku wa maombi, kwa kuwa, kama tulivyokusanyika, tukijua ya kwamba walipo wawili ama zaidi wamekusanyika pamoja, Wewe utakuwa pamoja nasi. Nasi tunakuomba Wewe, Bwana, utupe Neno Lako usiku wa leo. Nena nasi, Bwana, na uipashe moto mioyo yetu, isivyo kawaida, kusudi tujue jinsi ya kujiadibisha kwa ajili ya wakati mkuu ulio mbele, kwa kuwa tunaamini ya kwamba tunakaribia Kuja kwa Bwana.

³ Tunakushukuru kwa ajili ya watu sasa wanaoanza kuona imani kuwa ni ya thamani kwao, na kujua maana ya imani. Na tukijua, hata kukushukuru kwa ibada ambazo zingali mbele, tukiamini ya kwamba utafanya jambo fulani. Bwana, tunangojea kwa hamu, kama zile siku za kale, tukiamini ya kwamba wakati umekaribia ambapo Wewe unakaribia kuyafungua madirisha ya Mbinguni na kumwaga ahadi ambazo Mungu ameahidi katika siku hii ya mwisho.

⁴ Sasa tunakuomba Wewe, Bwana, ku—kuwa pamoja na wote, kote kote katika mataifa, kwa kuwa leo tulisikia wengi sana hapa, kila mahali, walio wahitaji. Wajalie haja zao, Bwana. Nasi tunaomba kuuona mkono mkuu wa Mungu ukitenda kazi kote duniani miongoni mwa wale ambao wanalitazamia jambo hili kuu.

⁵ Tusamehe dhambi yetu. Turudi, Bwana, kwa Roho Wako na Neno Lako, kusudi tujiadibishe, watumishi watiifu, watumishi watiifu katika mapenzi ya Mungu. Jalia tukumbuke, na tujaribu kuwaza mioyoni mwetu, yale Wakristo wa mwanzoni waliyofanya. Tungekutana na watu wa aina gani kama tulikutana na wale waliokuwa pamoja Nawe wenyewe. Jinsi ambavyo hapana shaka nyuso zao zilinawiri kwa imani na furaha. Jinsi hapana shaka maisha yao yalikuwa ni Neno la Mungu lililo hai, “nyaraka halisi zilizoandikwa zinazosomwa na watu wote,” walipokuwa wakitembea kati na miongoni mwa watu. Mungu, tujalie mara nyingine tena.

⁶ Jalia maisha yetu yasalimishwe sana Kwako, hata Roho Mtakatifu Mwenyewe ataishi kupitia kwetu, katika

kunena kupitia sisi, Bwana. Jalia tukumbuke, niani mwetu, tunapotembea barabarani na kugusana mikono na walimwengu, haitupasi kuwa kama hao. Nasi tunasimama kando na kuwapa mahali, Bwana, katika mahali pao panapofaa hapa duniani. Tutachukua kiti cha nyuma, tukijua ya kwamba sisi ni wajumbe kutoka ulimwengu mwingine. Tuna ufalme unaokuja mamlakani, Bwana. Na Mfalme wetu mkuu atawasili hivi karibuni na kuchukua mamlaka juu ya falme zote zilizo katika milki Yake. Naye atatawala na kumiliki; pamoja Naye hapa duniani, miaka elfu moja, na tuwe Naye milele.

⁷ Tukiwa na hili moyoni, Bwana, sasa tunatarajia jibu la maombi yetu. Tunayatazamia maungamo yetu. Endapo tumefanya jambo lolote, kusema chochote, ama kuwaza chochote, ambacho ni kinyume na mapenzi Yako mkuu, jalia Damu ya Yesu Kristo itusafishe.

⁸ Tuongoze, Bwana, kama yule dada alivyosema usiku wa leo, kuhusu yeye na mume wake wakienda zao Chicago. Waongoze, Bwana Mungu, hadi mahali ambapo unaweza kutumia, wapate kuwa miali ya nuru kwa wengine wanaopapasa-papasa gizani, wasiomjua Bwana wetu Yesu. Sasa tunaikabidhi ibada Kwako, na kulisikiliza Neno Lako la marekebisho, ili tupate kujua jinsi ya kujiandaa kwa ajili ya wakati huu mkuu, katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

[Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu Neville anafafanua—Mh.]

Bwana akubariki. Asante, ndugu.

⁹ Kidogo sikutarajiwa kwa jambo hili. Mimi, nikiwa hapa nyumbani, nilijisikia kama kwamba ikiwa haikunibidi kwenda mahali fulani, dharura, ningejisikia vibaya sana, mimi kuketi nyumbani wala nisije kwenye mkutano wa maombi. Na kwa namna fulani nikapitia hapa, bila kutarajiwa, kwangu mwenyewe, hata kwa familia yangu. Nimeingia sasa hivi, kisha nikaondoka mara moja. Na kwa hiyo nilisema, “Ninashuka kwenda kwenye mkutano wa maombi.” Na mke hata hakupata wakati wa kujitayarisha kuja, kwa hiyo yeye hakujua nilikuwa nikija.

¹⁰ Kwa hiyo ninafurahi kusikia ushuhuda wa dada hapo, huyo ndugu, juu ya hiyo Nuru huko Carolina ya Kusini ama Carolina ya Kaskazini, mahali fulani. Greenville, sivyo? [Dada mmoja anasema, “La. Pines ya Kusini.”—Mh.] Pines ya Kusini. Naam.

¹¹ Ndugu Lee Vayle alikuwa tu hapa leo. Nilibatiza, leo, katika ibada ya ubatizo hapa leo. Ndugu Lee Vayle mnamjua, na wahudumu pale, Ndugu Parker Thomas. Kuna . . .

¹² Ninakumbuka wa—wakati, dada fulani akiwa ametiwa uvuli. Ilikuwa ni thibitisho kubwa, dada, ya yale. . . Roho Mtakatifu wakati mwingine atatuacha tuendeleo na kuijaribu imani yetu, kuona nini, na kuijaribu imani ya wengine.

Unapoangalia kitu fulani moja kwa moja na unaona kitu fulani na useme hivyo; wengine wanaangalia wala hawakioni, wanasema hakipo. Unaona? Lakini kipo.

¹³ Sasa, hakuna mtu angaliweza kuiona ile Nuru iliyokuwa ikining'inia juu ya Paulo, lakini ilikuwapo. Hakuna mtu aliyemwona yule hua akishuka kutoka Mbinguni, katika ile Nuru, katika umbo, na ikaning'inia juu ya Yesu, ila Yohana mwenyewe. Bali ilikuwapo. Unaona?

¹⁴ Na kwa hiyo, basi, baadaye wakati nilipokuwa nikiwaambia watu kuhusu Nuru hii ikiwa kama Nguzo ya Moto, hakuna mtu aliyetaka kuamini hilo. Lakini sasa jicho la kimitambo la kamera lilitambulisha Hiyo, jinsi ilivyokuja.

Na pepo mchafu ni mweusi.

¹⁵ Ni kama tu maisha yetu, sisi ni vivuli. Nasi ni. . . Ikiwa sisi ni nuru, ambapo kama maisha yetu yakikubaliana na Nuru ya siku hizi, tunatembea katika Nuru.

¹⁶ Ni kama tu vile unavyoangalia nje na kusema, “Ninaliona jua,” mchana. U—unaona kivuli cha jua. Ni uakisi wa jua. Si jua, lenyewe, bali inathibitisha ya kwamba kuna jua. Inathibitisha ya kwamba kuna jua.

¹⁷ Na sasa ninapoona, kama ninyi mnaoketi huko nje, mkitumia feni, mkizungumza, hilo lina maana kwamba mko hai, bali ni kivuli tu cha uhai.

¹⁸ Kwa sababu, kitu chochote hakina budi kuwa na giza ndani yake, kipate kufanyiza kivuli. Mnaona? Kwa kuwa, kivuli kinapaswa kuwa na kiasi fulani cha giza na kiasi fulani cha nuru, kufanyiza kivuli. Wala hakiwezi kuwa ni giza tupu, na hakiwezi kuwa ni nuru tupu. Kama ni giza, ni giza tupu kweli. Kama ni nuru, hakuna kivuli, hakuna kitu cha kufanyiza kivuli. Lakini kama kimechanganyana na giza na nuru, inafanyiza kivuli.

¹⁹ Kwa hiyo kweli sisi ni vivuli vya nuru. Sasa wewe unaakisi uhai kutoka mahali fulani. Kama unaakisi, na ni Mkristo, hiki kikiwa ni kivuli, inathibitisha tu kwamba kuna Uhai mahali ambako huwezi kufa, kwa kuwa maisha haya yana mauti ndani yake. Unaona? Bali ni kivuli, kwa maana wewe ni kiumbe hai, kinachotembea kilicho na uwezo wa kuona, kuwaza, kusogea, na kuzungumza, chenye zile hisi tano za mwili. Lakini hata hivyo unajua, wao, wao wanakufa. Na kuna matatizo mengi sana. Unajua, yanaweza tu kuwa ni. . . Ni uakisi, unaona, ya kwamba kuna uhai na mauti yaliyochanganyikana pamoja.

²⁰ Mwili hauna budi kufa. Lakini kama unaakisi, kwa maisha yako yapatikanayo na mauti, Nuru ya Mbinguni, basi unauakisi Uzima wa Milele, Mungu. Ndipo utakapokufa, huwezi lingine ila kwenda kwenye Nuru hiyo, kwa maana Hiyo ndiyo umeakisi.

²¹ Kama wewe ni wa ulimwengu wa giza, unauakisi huo, na unaweza, huwezi kwenda kwingine ila gizani. Unaona? Kwa hiyo

tuko katika uakisi. Kwa hiyo, tunaona jambo hilo. Na hakika tu kama vile Roho Mtakatifu anavyoakisi Nuru na Uzima, vivyo hivyo nayo mauti huakisi giza.

²² Na hayo hapa yote mawili. Kesh-... Ifikapo mwisho wa juma hili, labda ifikapo Jumapili, tutaipanua ile picha ndogo kuifanya saizi kubwa, ipate kuwekwa kwenye ubao wa matangazo.

²³ Ambapo, picha *yenu* imetundikwa pale kwenye ubao wa matangazo. Sijui kama mliiona, ama hamkuiona. Na ndipo. . .

Na karibu juma moja lililopita, huko—huko Jamaica, ambako nilikuwa nikifanya umishenari. Tunatuma kanda kote ulimwenguni. Na *Ile Mihuri Saba* imefika huko. . . huko mbali katika visiwa vya Jamaica, huko ndani kabisa. Na kuko nyuma sana kule, nyuma ya Mlima wa Bluu. Nao wenyeji, wakati mwingine, wana ki—kinasasauti tulichowapa, ambacho inakubidi ku—kuninii, kama ile Santuri ya kale, unazungusha mpini wake, halafu una—unakiacha kicheze namna hiyo. Halafu, kila dakika chache, itambidi mtu kuzungusha mpini.

²⁴ Kundi hili lilikuwa na be—betri ndogo, betri ya volti sita, ama kitu kama hicho, ya kuchezea kinasasauti hicho. Nao—nao wote walikuwa wameketi pamoja, kama vile ilivyo hapa usiku wa leo, wakiisikiliza hiyo *Mihuri*, ninaamini ndivyo ilivyokuwa. Na wakati nilipokuwa nikinena, waliona, ikija humo chumbani, Nguzo ile ile ya Moto ilikuja, ikasogea mahali kinasasauti kilipokuwa na ikashuka kutulia juu yake. Nao wakaondoka wakaenda wakachukua kamera na kuipiga picha. Na ni ile ile, Ile pale, imening'inia pale juu yake. Sasa tutaipanua, kusudi tuiweke kwenye ninii—ubao wa matangazo pale nje, mpate kuiona.

²⁵ Tunashukuru sana kwa neema hiyo ya Mungu ambayo imeletwa ndani ya ninii yetu. . . imetuleta Mbele Zake katika siku hizi. Sasa tunashukuru kwa ajili ya mambo mengi.

²⁶ Sasa nafikiri nitaangalia hapa ndani nione kama ninaweza kupata baadhi, baadhi ya mihtasari ama ninii, chochote kile nilichozungumzia. Ama, tupate namna fulani ya—ya. . . Nina fungu lililoandikwa hapa, haidhuru, hapa nyuma katika kitabu. Kama ninaweza kupata moja, labda Bwana atanipa jambo fulani la kusema juu ya kitu fulani, wakati tukiomba.

Sasa tuna matarajio kwa ajili ya Jumapili.

²⁷ Nimekuwa nikizungumza katika Jumbe. Na, Jumapili, niliaweka hapa kwa muda mrefu, juu ya, “Mbona unanililia? Nena na watu na msonge mbele.”

²⁸ Sasa, Jumapili ni ibada ya uponyaji ambapo wagonjwa wataombewa. Sasa, mtu ukiwaendea wagonjwa, na hapana budi pawe na sababu kwamba wagonjwa, tunapowaombea, kama hawaponi. Nami ninataka, Bwana akipenda, kwa ajili ya somo

dogo tu Jumapili asubuhi, pia. Kwa hiyo, nitakuwa na ibada ya uponyaji, na kuwaombea watu wote. Na Billy Paul ama baadhi yao watakuwa hapa Jumapili asubuhi, kama saa mbili, kanisa litakapofunguliwa, kuwapa watu kadi wanapoingia mlangoni, ama wakati wowote watakapoingia.

²⁹ Na sasa, basi, ninataka kujaribu, ninaamini Bwana kwa namna fulani amenipa ufahamu mdogo juu ya sababu ya kuwako na watu wasioponywa. Nami ni—ninaamini ni kutokufahamu. Pia mimi—naamini, pengine, tutazungumzia jambo hilo. Jumapili asubuhi, Bwana akipenda.

³⁰ Sasa, mkutano wa maombi wa Jumatano usiku ni mkutano mfupi tu ambapo tunakutanika na kuomba, kama tulivyofanya, na kushirikiana.

³¹ Wakati mwingine, mimi—ninaamini moja ya mambo makuu ninayopata siku hizi, ni ukosefu wa uaminifu wa yale tunayoamini. Unaona? Unaona? Kama Mungu, katika siku za John Wesley, angalifanya siku hiyo vile amefanya leo, ingekuwaje; katika siku za Martin Luther, ama ye yote yule? Kama vile tunavyomwona akifanya, ambayo yamethibitishwa na Kanisa, na Roho; pia na sayansi, na kila hatua, ninii—emalshani yake haina budi kutambua. Nalo Neno la Mungu hapa likilitangaza na kulisimulia kabla halijatukia. Na halafu akija juu, na kutabiri, na kuonyesha jambo lile hasa alilosema. Litatimia kikamilifu, vile vile hasa Yeye alivyosema. Na bado tunaketi kwa namna fulani wazembe, kana kwamba tunashangaa. “Vema, sijui kama hilo lingemaanisha kwamba ni mimi? Sijui kama ingemaanisha tu ka—kanisa, kwa jumla. Ama—ama, sijui kama kweli nimehesabiwa katika jambo Hili?” Nafikiri, Jumapili asubuhi, nitajaribu kuzungumza juu ya baadhi ya mambo hayo muhimu ambayo huenda yakatuelimisha kidogo.

³² Sasa, usiku wa leo, nilipata jambo fulani, nililifungua tu hapa, kabla sijaja hapa. Nikawaza, “Vipi kama Ndugu Neville, kama ningefika kule chini na aseme, ‘Simama uhubiri,’ kisha aketi tu?” Mnaona? Nikawazia, “Afadhali niandike Maandiko machache.” Kwa sababu, ninajua, yeye, yeye ni ndugu mzuri sana, na sisi—sisi tunamthamani.

³³ Kabla hatujaomba kuhusu Neno, ninataka kuwajulisheni ndugu m—mmoja. Siwezi hata kukumbuka jina lake wakati huu, wawili wa hao. Wako hapa, marafiki zangu. Ninii. . . Wao ni wahudumu na wainjilisti, hudumani, wakitoka. Walizisikia Jumbe hizi kwa kanda. Nao wametoka katika makanisa mbalimbali ya kimadhehebu, jamaa wawili wadogo. Na mvulana huyo ananinii sana, mmoja wao alishawishika sana, hata akaruka akaja, Tucson, hivi majuzi, mkutano ulipokuwa ukimalizika. Ninaamini nilikuwa kwenye Kiamshakinywa cha

Wafanya Biashara. Na jamaa huyo mdogo, jamaa mzuri mdogo, akashuka akaja. Naye ni . . .

³⁴ Wametoka Kansas. Nao wamekuja toka huko kote ili mimi nipate kuwaoza. Ninathamini hilo. Kuwazia ya kwamba wapo watu ambao wanaamini maombi yako, vya kutosha, wanaamini ya kwamba Mungu angeyasikia maombi na kuyajibu; vijana wakianza maisha, namna hii. Nao walipofika hapa nipate kuwaoza, jana, tuliona sheria ya jimbo la Indiana inaagiza, na hata ingawa wamefanyiwa uchunguzi wa damu, wangoje humu jimboni, siku tatu, kabla hawajafunga ndoa. Kwa hiyo, hawawezi kufunga ndoa mpaka Ijumaa asubuhi.

³⁵ Nami nitamwomba ndugu yetu pale mwisho, kama atasimama tu na kutwambia kwamba yeye ni nani, na mchumba wake mpenzi pale, na ndugu huyo mwingine.

³⁶ [Ndugu huyo anasema, “Asante, Ndugu Branham. Nimejaliwa kuwa hapa. Nami ni . . . Mimi na Ndugu Roger tunaishi Kansas, huenda hudumani, kama mwinjilisti, tukitangaza, ‘Yesu huokoa, huponya, kwa imani katika Yesu . . . ? . . .’ Daima mimi hubeba . . . ? . . . Huyu ni mchumba wangu, Patricia Brown. Tutafunga ndoa, Ijumaa. Mwinjilisti na mfanya kazi mwenzangu, Ndugu Ronnie . . . ? . . . hapo mwisho. Na Bw. Peetree kwenye ninii ile ile . . . ? . . .”—Mh.]

³⁷ Asante, sana. Hakika tunawatakia mabalozi hawa wachanga, kwa ajili ya kazi ya Bwana Yesu, Baraka za Mungu, kuwafanikisha njiani. Na kama nilivyokuwa nikijiuliza, nikingojea Kuja kwa Bwana, na kuwaona vijana wanaume na wanawake wakiwa na kusudi moyoni, kumtumikia Kristo, hilo linanifurahisha sana, unaona, kuwaona wakisimama namna hii. Bwana awabariki, sana, ndugu yangu, dada.

³⁸ Sasa hebu na tufungue kwenye Kitabu kidogo ambacho sijapata kuhubiria hapo kabla, maishani mwangu. Na ni ninii sana . . . Mlango mmoja tu, Kitabu cha Filemoni. Na ni ninii . . .

³⁹ Mimi kidogo tu ni Muairishi, nami—nami nina waya uliolizunguka jino langu la chini, kushikilia baadhi yake mahali pake huku nyuma. Wakati mwingine siyatamki majina haya vizuri, wakati nikijua yalivyo. Na wakati mwingine siwezi kuyatamka vizuri, kwa sababu ya ukosefu wa elimu. Kwa hiyo, “Filemoni,” mtu fulani alisema huko nyuma, ambalo nafikiri ndilo tamshi lake sahihi.

⁴⁰ Sasa, kifungu cha 1, ninataka kuchukua neno moja tu ama mawili kutoka kwake.

Paulo, mfungwa wa Yesu Kristo, . . .

⁴¹ Na hilo ndilo ninalotaka kutumia usiku wa leo, kama fungu la maneno, Bwana akipenda, ni: *Mfungwa.*

42 Sasa, ingekuwa ni vigumu kwako kumwazia Paulo akijihesabu kama mfungwa. Mtu aliyezaliwa huru, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, bali hata hivyo anajiita “mfungwa.”

43 Na sasa tunaona, wakati anapozungumza na Wakorintho, “Paulo, mtume wa Yesu Kristo.” Wakati mwingine, “Paulo, mtumishi wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu,” wakati akizungumza na Timotheo, watu mbalimbali. Sasa wakati anapomwandikia Filemoni hapa, yeye alisema, “Paulo, mfungwa wa Yesu Kristo.” “Paulo, mtume,” ningetaka kuhubiri usiku mmoja juu ya hilo. “Paulo, m—mtumishi,” kuhubiri juu ya hilo. Na kisha, “Paulo, mfungwa.”

44 Lakini, usiku wa leo, kwa kuwa ingechukua saa kadhaa kutafakari moja ya masomo haya ipasavyo, ningetaka kuchukua, usiku wa leo, “Paulo, mfungwa,” na kuchukua somo la: *Mfungwa*.

Sasa na tuinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

45 Bwana Yesu, mtu yeyote, ambaye ana uwezo wa mwili, anaweza kufungua kurasa za Biblia hii, bali Roho Mtakatifu Ndiye tu anayeweza kuifasiri katika nuru iliyokusudiwa. Tunamwomba aje sasa na atusaidie kufahamu kile hili lilichokuwa, lilichoelekezewa, huyu Paulo, huyu nabii mkuu, mwenye nguvu, na hata hivyo anajiita “mfungwa.” Naomba Roho Mtakatifu atufunulie jambo hili tunapomngojea, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

46 Sasa naweza kuwazia, Paulo, wakati alipomwandikia Filemoni barua hii, jinsi alivyokuwa ameketi gerezeni, huko chini kwenye korokoro la jiji hili, m—m—mfungwa. Naye angeweza kufahamu vizuri, katika hali yake kile neno hilo lilichomaanisha. Alikuwa amezungukwa na—na—na nondo za chuma. Yeye—yeye angeweza tu kuwekwa huru wakati mtu akimweka huru. Naye alijua ilichomaanisha kuwa mfungwa. Halafu basi, tena, ninaamini ya kwamba m—mtume huyo alimaanisha kidogo tu. . . sio hasa kulielekeza kwenye hali yake ya sasa, ya kuwa mfungwa wa utu wa—wake wa kimwili uliokuwa hapa katika hii—katika jela hili. Lakini ninaamini alikuwa akirejea kwenye utu wa—wake, roho wa—wa—wake, mapenzi yake, kuwa mfungwa wa Yesu Kristo.

47 Sasa, sisi sote tumezaliwa, wenye hiari huru, kufanya uamuzi wowote tunaotaka. Mungu hufanya hivyo kwa haki. Kwa maana, Yeye hana budi kumweka kila mtu kwenye msingi ule ule, vinginevyo alimweka mtu asiyefaa kwenye. . . Alimweka mtu wa kwanza juu ya msingi usio sahihi, ambaye alimweka kwenye uhuru wa kujichagulia. Unaona? Tuko vile vile kabisa, usiku wa leo, kama Adamu na Hawa. Hakuna tofauti. Mema na mabaya yamewekwa mbele ya kila mmoja wetu. Uzima na mauti, tunaweza kujichagulia; ni juu yako, kujichagulia. Unaona?

48 Hivyo ndivyo Adamu na Hawa walivyofanya, na, mnaona, na—nao walifanya uamuzi mbaya. Na sasa, kwa njia hiyo, wakaweka jamii yote, ya jamii ya binadamu, chini ya mauti, adhabu ya kifo.

49 Na ndipo basi Mungu akashuka katika mfano wa mwanadamu na kuichukua hiyo mauti, na kuilipa adhabu ya mauti, ili ninii. . . Raia Wake waliopenda ku—kuwa huru wangeweza kuwa huru.

50 Sasa, kama Yeye alituchukua, pasipo kutumia njia ile ile aliyowachukua Adamu na Hawa, atuvute kupitia kitu fulani, aseme, “Nitawaokoa mpende msipende,” basi Yeye alimweka Adamu na Hawa juu ya—juu ya msingi usio sahihi, mnaona. Lakini kila mmoja wetu hana budi kujichagulia, leo hii, kati ya mauti na uzima. Tunaweza kuchagua.

51 Kama vile nilivyosema sasa hivi, iwapo nuru yako itathibitisha, maisha yako yatathibitisha kwamba wewe hasa uko upande gani. Sijali wewe unasema uko upande gani. Yale unayofanya, kila siku, yanathibitisha kile ulicho. Umesikia ule msemu wa kale, “Maisha yako yananena kwa sauti kubwa sana, siwezi kuusikia ushuhuda wako.” Unaona? Matendo yako—yako yananena kwa sauti kubwa sana.

52 Daima nimeamini katika kupaza sauti na kuruka-ruka. Lakini daima nimesema, “Usiruke juu zaidi ya unavyoishi, maana ulimwengu utaliangalia jambo hilo.” Unaona? Inakupasa kuruka juu kadiri tu unavyoishi, kwa hiyo, kwa kuwa mtu fulani anakuangalia. Na sasa wakati. . .

53 Watu hawatakuja kanisani. Wao—wao, wengi wao, kamwe hawatakuja. Na baadhi yao, wasiokuja, ni watu waaminifu. Wameona upotovu mwingi sana kanisani, mpaka hawataki kuwa na uhusiano wowote na jambo hilo. Na mara nyingi, tunanena juu ya wazo wazi la hilo, ni vigumu kwako kuwalaumu, unaona, kwa sababu ya—ya jinsi watu wanavyotenda. Wanajiita Wakristo. Hao ndio jiwe kuu sana la kujikwaa ambalo ulimwengu unalo, ni mwanamume na wanawake wanaokiri kuwa mtu ni Mkristo, na anaishi tofauti na wanavyokiri. Kweli kabisa.

54 Sasa, kwa kuwa maudhi yatatokea kwenye ile Hukumu. Sasa, mwenye dhambi, mwuza pombe haramu, mcheza kamari, mzinzi, yeye—yeye hataabika kusikia hukumu yake ikisomwa, “Kuondoka aingie kwenye moto wa milele.” Hatatahayari. Bali huyo jamaa anayejaribu kujificha nyuma ya namna fulani ya maungamo ya kanisa, huyo ndiye mvulana atakayeudhika kwenye Siku ya Hukumu. Unaona? Ambaye anakiri kuwa Mkristo, naye anaishi vinginevyo. Ingalikuwa ni afadhali kwake kama kamwe hata hakufanya namna yoyote ya maungamo, hakuanza, kuliko kuanza na kuishi kitu tofauti. Kwa sababu, yeye ndiye jiwe kuu sana la kujikwaa tulilo nalo, ni kwa

huyo mtangaza-imani anayesema kwamba yeye—yeye—yeye ni Mkristo, naye anaishi vinginevyo.

⁵⁵ Daima, usiyapime maisha yako kwa kadiri ya nguvu ulizo nazo za kufanya miujiza. Wala hatujipimi kwa kiasi cha maarifa uliyo nayo ya Neno. Bali daima jipime, rejea nyuma na uchukue mahesabu ya aina ya tunda ambalo maisha unayoishi kwa sasa yanazaa. Unaona?

⁵⁶ Kama nilivyohubiri wakati fulani uliopita, kwenye mkutano wa wafanya biashara huko Phoenix, Arizona, juu ya uakisi wa Yesu, kuyaakisi maisha ya Mkristo. Nilisema nilizaliwa hapa juu Kentucky, ambako hakuna ustaarabu kabisa, hasa sana wakati nilipokuwa mtoto mdogo. Na kijana fulani huyu kamwe hakuwa na nyu—nyu—nyu—nyumba kama tulizo nazo hapa, ambapo tulikuwa na mama wengi sana warembo ambao inawabidi kujiangalia kwa vioo, kote nyumbani, kuweka tu nywele zao jinsi inavyopendeza, na kadhalika. Lakini alikuwa na kioo kimoja kidogo, kipande kidogo tu kilichotundikwa nje mtini, ambapo ubao wa kunawia ulipokuwa, ambapo mama yake na baba walina, na wakachana nywele zao, na kadhalika, kutokana na kipande hiki kidogo cha kioo cha kale kilichotundikwa mtini.

⁵⁷ Kusema kweli, hiyo ndiyo aina ya nyumba tuliyo nayo. Mtu yeyote anayetaka kukiona kioo, sisi watoto, ilitubidi kuchukua sanduku na kupanda kwenye benchi la kunawia, na kujiangalia kwenye kipande hiki cha—cha kioo nilichookota, mimi mwenyewe, kwenye jalala. Hiyo haikuwa ni huko chini Kentucky. Hiyo ni hapa Indiana, juu kwenye Utica Pike hapa.

⁵⁸ Sasa, maskini mtoto huyu hakuwa hasa amejiangalia mwenyewe jinsi hiyo. Kwa hiyo, akaja mjini, kumtembelea bibi yake. Na kwenye ninii. . . Ni katika kuzunguka na kutazama nyumba, bibi huyo alikuwa na nyumba ambayo ilikuwa na kioo kizima mlangoni. Na kwa hiyo, mvulana huyo mdogo, akikimbia kupitia chu—chumbani, alimwona mvulana mwingine mdogo mbele zake. Naye mvulana huyo alikuwa akikimbia, pia. Kwa hiyo akawazia anapaswa kusimama kwa dakika chache aone yale mvulana huyo mdogo aliyotaka kufanya. Na aliposimama, huyo mvulana mdogo akasimama. Alipogeza kichwa chake, mvulana huyo mdogo akakigeza kichwa chake. Akakuna kichwa chake, huyo mvulana mdogo akakuna chake. Hatimaye, akasogea karibu, apate kuchunguza. Kisha akageuka. Naye mama yake akimtaazama, na bibi yake, kwa mshangao. Kasema, “Lo! mama, yule ni mimi.”

⁵⁹ Kwa hiyo nikasema, ya kwamba, “Sisi, pia, tunaakisi kitu fulani.” Mnaona? Maisha yetu yanaakisiwa.

⁶⁰ Na sasa, kama tuliishi katika siku za Nuhu, je! tungechukua upande wa nani? Tungechukua upande gani katika siku hiyo kuu ambayo Nuhu aliishi? Tungechukua upande gani katika siku za Musa? Ni upande gani katika siku za Eliya, yule nabii,

wakati ulimwengu mzima ulipokuwa umemezwa katika mambo makuu ya—ya kisasa, kama vile Yezebeli mamboleo, na ulikuwa umewatwaa watumishi wote wa Bwana ukawaingiza katika mambo ya kilimwengu? Nalo kanisa pamoja na makuhani walikuwa wakimsujudu. Je! ungechukua upande wa kupendwa na watu, ama ungalisimama na Eliya?

⁶¹ Sasa, na katika siku za Bwana Yesu, wakati tungewazia juu ya Mtu huyu asiyependwa na watu, asiyeelimishwa na ulimwengu, wasingeweza kupata shule zozote alizopitia, wala hana—hana ujuzi wa seminari. Ha—halafu anasimama kwa jina la “kuzaliwa kiharamu.” Kisha anatoka, akihibiri Injili ambayo ilikuwa ni kinyume na chochote walichokuwa wamefundishwa. Ninii sana. . . Na kuwakemea wahudumu na madhehebu yao, na kadhalika.

⁶² Nayo madhehebu yalikuwa yametoa ka—ka—kauli, “Kama mtu yeyote akienda kumsikiliza huyu anayejiita nabii, angefukuzwa kwenye sinagogi,” ambayo ilikuwa ni—ni dhambi ya kufisha. Iliwabidi wawajibike. Njia pekee wangaliweza kuabudu ilikuwa ni chini ya damu ya mwana-kondoo. Ilibidi kuijia dhabihu hii. Na—na halafu walitengwa, na lilikuwa ni jambo kubwa jinsi gani.

⁶³ Naye mtu huyu akapuuza mambo kama hayo. Na hata hivyo alikuwa pamoja na Maandiko kikamilifu, bali si kwa njia ile wao waliyoyajua. Je! ungechukua upande gani? Unaona? Sasa, usininii. . . Maisha yako unayoishi sasa, yanaonyesha sasa kile hasa ungalifanya wakati huo, kwa sababu ungali una roho yule yule. Unaona? Ukichukua upande huo sasa, pamoja nao, ungalifanya hivyo wakati huo. Kwa kuwa, roho yeye yule aliyenndani yako sasa alikuwa ndani ya watu wakati huo. Unaona?

⁶⁴ Ibilisi kamwe hamwondoi roho wake; yeye huenda tu kutoka mtu mmoja anaingia kwa mwingine.

⁶⁵ Wala, Mungu kamwe hamwondoi Roho Wake; huenda toka kwa mmoja hadi kwa mwingine. Unaona?

⁶⁶ Kwa hiyo, Roho yeye yule aliyekuwa juu ya Eliya alikuja juu ya Elisha, yeye yule aliyekuwa juu ya Yohana Mbatizaji, na kadhalika.

⁶⁷ Roho Mtakatifu, aliyekuwa juu ya Kristo, alikuwa juu ya wale wanafunzi, kotekote, na angali juu ya watu. Unaona? Mungu kamwe hamwondoi Roho Wake.

Kwa hiyo sisi hao hapo tumeachwa, kujiamulia.

⁶⁸ Wala si—siwezi kuona hapa mahali ambapo Paulo alikuwa akijutia chochote, na kusema ya kwamba alikuwa anasikitika yeye alikuwa ni mfungwa. Lakini alikuwa akijieleza. . . Ninaamini ya kwamba Paulo, wakati akiandika waraka huu kwa kalamu ile, ya kwamba Roho Mtakatifu Ndiye aliyemfanya kuandika hayo. Kwamba, labda, hata kwenye

usiku huu, ya kwamba tupate kutoa muktadha wa fungu letu la maneno, kuonyesha ni kwa nini Paulo alifanya jambo hili. Kwa sababu, ni la Kimaandiko, na la Kimaandiko ni la Milele. Ninaamini, ya kwamba, wakati akiketi kwenye maskini jela hii chafu sana, kwamba Paulo alimwandikia mwenziwe hapa, ya kwamba, ndugu yake, ya kwamba yeye alikuwa ni “mfungwa wa Yesu Kristo.” Kwa hiyo, angeweza kulielezea kwa kuona yale yaliyomzunguka. Sasa, yeye alikuwa gerezani, bali hilo silo alilokuwa akizungumzia, mtumishi hu—huyu wa Kristo, mhudumu mwenzake. Yeye alikuwa akisema ya kwamba alikuwa ni mfungwa kwa Neno la Yesu Kristo, maana Kristo ni Neno.

⁶⁹ Na Paulo alikuwa ni mwanachuoni mashuhuri sana katika siku zake. Alikuwa na lengo kuu. Alikuwa ni—alikuwa m—m—mtu aliyekuwa amefunzwa kwa ninii, na watu, jamaa fulani jina lake Gamalieli, ambaye alikuwa ni mwalimu mashuhuri wa siku yake, moja ya shule kuu sana ambazo angaliweza kuhudhuria. Kwa mfano, kama vile tunavyosema, Wheaton, ama Bob Jones, ama shule fulani kuu ya kimsingi. Alikuwa amefunzwa kama—kama—kama mhudumu wa Neno. Naye alikuwa na elimu nzuri, na ni mwenye bongo, na mvulana mwenye akili akiwa na lengo kuu la labda siku moja kuwa kuhani ama kuhani mkuu kwa watu wake.

⁷⁰ Alikuwa na lengo. Halafu tunaona, ya kwamba, lengo hili kubwa alilokuwa amefundishwa kwa ajili yake, na aliyokuwa ametumia maisha yake yote, kutoka labda kwenye umri wa kama miaka minane ama kumi, mpaka kufikia karibu thelathini ama thelathini na mitano, wakati alipomaliza chuo na kuhitimu; naye alikuwa na diploma zake zote na kila kitu, na alikuwa na sifa nzuri kwa makasisi wo—wote, hata kwa kuhani mkuu huko Yerusalemu. Alikuwa na maagizo kutoka kwake, maagizo ya kibinafsi, yaliyoandikwa, yakaaminishwa kwa huyu Sauli mashuhuri, “Kushuka kwenda Dameski na kuwatafuta hao wote huko chini waliomwabudu Mungu kinyume na yale aliyosema, na kuwafunga na kuwaweka gerezani. Ikilazimu, alikuwa na amri ya kuwaua, kama angetaka.” Alikuwa...Alikuwa na lengo kuu.

⁷¹ Na sasa, yote aliyokuwa amefunzwa, Mungu aliyatoa yote kutoka kwake. Unaona? Na lililokuwa ni lengo lake, na kile baba yake alichokuwa ametumia pesa kwake, na shauku ya baba na mama yake, yote yaliondolewa kwake kwa kuwa—kuwa Mungu alikuwa na kitu kingine. Kwa hiyo, yeye alikuwa ni mfungwa kutokana na lengo lake alilokuwa nalo maishani, naye alikuwa amefanyika mfungwa kwa Yesu Kristo, ambaye alikuwa ni Neno.

⁷² Ile barabara ya kwenda Dameski ilimbadilisha Paulo. Akienda zake, kama saa tano, labda, mchana, ambapo alipigwa akaangushwa chini. Naye akasikia Sauti, ikisema, “Sauli,

mbona wanitesa?” Ndipo akaangalia juu. Na alipoangalia juu, akiwa ni Myahudi, basi alijua ya kwamba hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa ni Bwana aliyewaongoza wana wa Israeli, kwa sababu yeye alijua hivyo ndivyo ilivyokuwa.

⁷³ Kumbukeni, Mwebrania huyu asingeweza kamwe kuita chochote “Bwana,” herufi kubwa za B-w-a-n-a, Elohimu, isipokuwa awe ameridhika kwamba hivyo ndivyo ilivyokuwa, kwa maana alikuwa mwanachuoni aliyefunzwa. Basi wakati alipoangalia juu, na kuiona Hii, Nuru, Nguzo ya Moto iliyokuwa imewaongoza watu wake kupitia nyikani, naye akasema, “Bwana,” Elohimu, herufi kubwa za B-w-a- . . . “Bwana, U Nani Wewe?”

⁷⁴ Basi ni mshangao wa jinsi gani uliompata mwanatheolojia huyu, kuambiwa, “Mimi ni Yesu,” yeye yule aliyekuwa akimpinga sana. Ni ninii—ni badiliko la jinsi gani! Loo! Loo! Hapana budi lilikuwa ni jambo la kutisha kwa mtu huyu, kwamba jitihada zake zote alizokuwa nazo, kutaka kujua, mara moja, alikuwa akimtesa. Malengo yake yalikuwa yamemsukuma mba—mbali sana kutoka kwenye jambo muhimu alilotaka kufanya. Na ulikuwa hapana budi ni mshtuko m—mkubwa jinsi gani, kwa mtume huyu, wakati Yeye aliposema, “Mimi ni Yesu,” yeye Yule aliyekuwa akimtesa. “Mbona wanitesa?”

⁷⁵ Nukuu nyingine ndogo tunayoweza kuingiza hapa ndani. Mnaona, wanapolidhiki Kanisa, si Kanisa hasa wanalodhiki, wanamdhihiki Yesu. “Mbona unanitesa?” Paulo angewezaje basi, pamoja na elimu yake yote, kuamini Huyu alikuwa ni . . . ya kwamba Kundi hili alilokuwa akilitesa lilikuwa ni Mungu yeye yule yeye alidai anatumikia? Nafikiri hiyo ni, bila kuingia katika utondoti, nafikiri sisi sote tumefundishwa vizuri vya kutosha kujua kile ninachomaanisha hapa. Jambo lile lile linatendeka leo.

⁷⁶ Paulo, kwa kutokujua, ingawa alikuwa ni mtu mwenye akili na mwerevu, mwerevu sana kuliko hao Wagalilaya wasioelimika alikuwa akiwatesa, ambao tayari katika unyenyekevu wao walikuwa wamemkubali Mtu huyu kama Bwana. Lakini, Paulo, katika mafundisho yake makuu na akili zake, asingeweza kukubali Hilo. Na jinsi ilivyokuwa ni mageuzi makubwa kwake, humu barabarani. Naye alipigwa kwa upofu, hivi kwamba asitekeleze agizo lake, bali aliongozwa akapelekwa mahali penye barabara fulani iliyoitwa Nyofu, na nyumba ya mtu fulani.

⁷⁷ Ndipo basi akashuka akaja nabii kule chini, jina lake Anania, ambaye aliona katika ono, yeye akija, akaona mahali alipokuwa, akashuka akaenda mahali alipokuwa, na akaingia ndani. Ndipo akasema, “Ndugu Sauli, Bwana aliyekutokea njiani ukija; amenituma, nipate kuweka mikono yangu juu yako, nawe upokee kuona kwako na ujazwe na Roho Mtakatifu.”

78 Angalia mahali alipokuwa. Jinsi—jinsi lilivyokuwa ni jambo kubwa sana kwa Paulo! Unaona? Yote aliyokuwa amefunzwa kufanya yalikuwa ni kinyume. Kwa hiyo sasa, pamoja na—pamoja na elimu yote aliyokuwa nayo, i—ilikuwa tu imekuwa ni bure kwake.

79 Sasa, yeye alijua ya kwamba alipata tukio. Kwa hiyo hili hapa somo lingine kwa ajili yetu, ya kwamba, tukio peke yake halitoshi. Inapaswa kuwa ni tukio kulingana na Neno la Bwana. Kwa hiyo, yeye alipoliona jambo hili, na kujua ya kwamba lilikuwa ni kitu Fulani kikuu, basi, kwamba mtu mwengine alikuwa amekipokea kabla yake, alichukua muda wa miaka mitatu na miezi sita huko chini ja—jangwani Arabuni; akichukua Bi—Biblia, kama ilivyokuwa wakati huo, Agano la Kale, na kushuka kwenda kule, ku—kulilinganisha tukio hili alilolipata, apate kuona kama lilikuwa ni la Kimaandiko.

80 Sasa vipi kama yeye alisema, “Vema, nadhani hicho kilikuwa ni kitu tu cha kupita,” na kuendelea na safari yake? “Nitafuata akili yangu?”

81 Sasa, ilimbidi afanywe mfungwa wa kitu fulani, mfungwa. Kwa hiyo baada ya kulilinganisha, na kuona, si ajabu angeweza kuandika Kitabu cha Waebrania, katika mfano. Unaona? Miaka mitatu na nusu huko chini, akidumu katika Neno, na kuona ya kwamba Mungu yeye yule aliyemwita alikuwa akimrudisha, na kubadilisha akili yake yote, akibadilisha yote aliyowahi kuwazia, yote aliyofunzwa kuwa. Lengo lake lote, lilifutiliwa kabisa mbali naye, naye akawa mfungwa. Upendo wa Mungu ulikuwa ni mkubwa sana, na u—ufunuo mkubwa sana, hata asingeweza kuachana Nao.

82 Hilo ndilo tukio la kweli la kila mwaminio wa kweli anayekutana na Mungu. U—unakutana na Kitu ambacho ni kikubwa sana, hata unaninii... hata—hata unakuwa m—mfungwa, kwa kitu chochote kingine. Unaona? U—unaacha kila kitu, upate kuwa mfungwa kwenye Hili.

83 Imeelezwa wakati mmoja ambapo Yesu alisema, “Ufalme wa Mbinguni ni kitu kama mtu kununua lulu. Ndipo anapoipata ile Lulu ya thamani kuu, anauza yote aliyo nayo, aipate Hiyo.”

84 Na hivyo ndivyo ilivyo hapa. Una—una dhana ya kiakili, una ujuzi wa ki—ki—ki—kitheolojia; bali inapofikia wakati u—u—unapopata Kitu kilicho halisi, u—unauza tu kila kitu kingine, nawe unajifungia kwenye Hiki.

85 Paulo alijua ilikuwa ni kitu gani. A—alikuta kwamba amefungiwa hatamu kwenye kitu Fulani. Kama vile tunavyomfunga fa—fa—farasi hatamu, ni ku—ni kuvuta kitu fulani. Na Paulo alijua, baada ya tukio hili, na miaka mitatu na nusu ya kulinganisha tu—tukio alilokuwa nalo, na Biblia, alitambua ya kwamba Mungu alikuwa amemchagua Naye alikuwa amemfunga kwa Roho Mtakatifu, tukio alilokuwa

nalo, kuvuta Injili kuileta mbele za Mataifa. Roho, Mwenyewe, alimfunga hatamu.

⁸⁶ Na, leo hii, kama watumishi wa Kristo, tunafungwa hatamu, tumefungwa. Hatuwezi kwenda. Tumefungwa Nalo, tukafungwa hatamu kwa Neno. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, wewe umefungwa hatamu Kwake. Kuna jambo fulani kulihusu Hilo, kwamba kamwe huwezi kuliacha. Umefungwa nira pamoja Nalo, kwa Roho Mtakatifu, amekufunga nira kwenye Neno. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, Ni Neno. Hilo daima limefungwa hatamu Nalo, limefungwa nira pamoja Nalo. Kwenye Neno, kwa Roho, yeye amefungwa hatamu.

⁸⁷ Yeye alikuwa amejifunza u—upande wa nyuma wa jangwa la Arabuni kule. Wakati, mambo yake yote ya awali, na ujuzi, na lengo, hayo, yeye alikuwa amevuliwa mambo hayo.

⁸⁸ Sasa, hapo ndipo tunapopata, siku hizi, ya kwamba hatuna budi kuvuliwa, kwanza. Nao watu hawataki kuvuliwa. Ndugu wa Kimethodisti anataka kushikilia kidogo mafundisho yake ya Kimethodisti. A-ha. Ndugu wa Kibaptisti anataka kushikilia kidogo mafundisho yake ya Kibaptisti. Unaona? Lakini inakubidi kuvuliwa kabisa kila kitu, na kuzaliwa tu mara ya pili, upya. Na uchukue kutoka hapo, umwache Roho Mtakatifu aongoze. Huwezi kusema, “Vema, sasa, baba ya—yangu alisema, wakati alipoingia, alipoenda kanisani, alipeana mikono na mchungaji. Yeye, yeye ni mfuasi mzuri mwaminifu.” Hilo huenda lilikuwa ni sawa kwa jamii yake, bali sisi ni jamii nyingine. Unaona? Sasa hatuna budi kurudi kwenye nyakati za Biblia kwa siku hizi.

⁸⁹ Makuhani walifungwa nira, pia. Lakini, unaona, walikuwa wameingia kwenye kipindi kingine cha wakati, na wao—wao wakashindwa kuvua hatamu yao ya kale na kujifunga kwenye hatamu mpya.

⁹⁰ Na ni jambo lilo hilo tunalopata siku hizi. Tulipitia kwenye wakati wa kimadhehebu, kama tulivyohitibisha katika nyakati za kanisa, Biblia, na kadhalika, bali tunakuja sasa kwenye wakati huru, ambapo Roho Mtakatifu Mwenyewe anashuka na kujithibitisha Mwenyewe, na kujitambulisha, anafanya kila ahadi aliyoahidi, kutimia. Loo, jamani! Ni wakati mkuu jinsi gani!

⁹¹ Naye alijua ya kwamba, jambo lingine, alijua asingeweza kwenda mahali mbalimbali. Kwamba, kwa kuwa amefungwa hatamu kwenye Hili, ya kwamba asingeweza, kwamba alininii, bali a—alitaka kwenda. Alijua ya kwamba shauku yake ilimvutia miongoni mwa ndugu zake ambako alialikwa kuja, na hata hivyo alisukumwa katika Roho kufanya jambo lingine. Yeye hakuwa ni mali yake mwenyewe.

⁹² Labda mtu fulani angesema, “Ndugu Sauli, Ndugu Paulo, tunakutaka uje huku, kwa sababu tuna kanisa lililo kubwa kuliko yote. Tuna kusanyiko lililo kubwa kuliko yote. Sadaka zako zitakuwa nyingi, na kadhalika.”

⁹³ Lakini akisukumwa sana katika Roho, yeye aliwazia, “Ninaye ndugu kule. Ningetaka kwenda kule na kumwokoia ndugu huyu, nimlete kwa Bwana.” Lakini, hata hivyo, Roho alimsukuma sana kwenda mahali pengine. Yeye alikuwa ni mfungwa. Kweli.

⁹⁴ Ee Mungu, tufanye wafungwa namna hiyo, kutoka kwenye lengo letu la ubinafsi, na kutoka kwenye maamuzi yetu wenyewe na mawazo yetu bora zaidi, tupate kuwa mfungwa wa Yesu Kristo. Nafikiri hilo lilikuwa ni tamshi kubwa, kwamba, “Mimi ni mfungwa wa Yesu Kristo.”

⁹⁵ Pia kumbukeni, Yeye ni Neno. Mnaona? Haidhuru mtu yeyote mwingine anawazia jambo gani, ni Neno. Unaona? Ikiwa wewe ni mfungwa wa Neno, hakuna dhehebu linaloweza kukutikisa kutoka kwa Hilo. Ni—ni Neno. Wewe ni ninii tu . . . Wewe ni mfungwa kwa Hilo, hivyo tu. Huna budi kutenda linavyotenda.

⁹⁶ Sasa, yeye asingeenda mahali fulani alikotaka kwenda, kwa sababu (kwa nini?) Roho alimkataza. Kumbukeni, mara nyingi, ambapo Paulo alikuwa akijaribu kwenda mahali fulani, akiwazia, “Huko ndiko ningeweza kufanya mkutano mkubwa,” lakini Roho angemkataza. Sasa, hilo kwa udhahiri linaonyesha na kuthibitisha ya kwamba Paulo alikuwa ni mfungwa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mfungwa wa Yesu Kristo, aliyetiwa hatamu kwa Neno Lake, kwa Roho! Loo! ninapenda jambo hilo. A-ha.

⁹⁷ Yeye alifungwa. Alifungwa kwa mnyororo, na kwa vifungo vya upendo, kufanya mapenzi ya Mungu, na hayo peke yake. Alikuwa ni mfungwa. Alikuwa katika vifungo vya upendo. Alikuwa amefungwa nira pamoja na Kristo. Asingeweza kufungiwa nira na kitu kingine chochote. Alikuwa amefungiwa nira pamoja Naye. Na mahali Uongozi ulipoenda, huko ndiko ilimbidi kwenda. Haidhuru malisho yalikuwa ni mazuri vipi, hapa upande *huu* ama upande *ule*, ilimbidi kwenda vile Kiongozi na nira walivyokwenda.

⁹⁸ Loo, usiku wa leo, ikiwa sisi, kama Maskani ya Branham, tungeweza tu kuwa wafungwa; kwa utu wetu wenye ubinafsi, kwa lengo letu, kwamba tungeweza kujitolea kabisa na kufungwa nira pamoja na Yeye, haidhuru ulimwengu unawazia nini, vile hao wengine ulimwenguni wanavyofanya. Tumefungwa kwa vifungo vya upendo. Sisi ni wafungwa. “Miguu yangu imefungwa nira sana kwa Kristo, haitacheza dansi. Macho yangu yamefungwa nira sana kwa Kristo, mpaka mimi, ninapowaona hawa wavua nguo mamboleo mtaani, Hilo

hukigeuza kichwa changu. Moyo wangu—wangu umefungwa nira sana katika upendo pamoja na Yeye, hata siwezi kuupenda ulimwengu huu, tena. Mapenzi yangu yamefungwa nira sana Kwake, hata sijui sasa malengo yangu ni yapi. Ni tu, ‘Uongozapo, mimi nitafuata, Bwana.’ Nitakuwa mfungwa.” Unaona?

⁹⁹ Paulo alikuwa ni mfungwa kwelikweli. Hakuwa akitoa tamshi lolote lisilo sahihi. Alifunzwa na Roho Mtakatifu, vilevile, kulingojea Neno. Sasa, alikuwa amefundishwa kwa njia fulani, bali—bali Mungu alikuwa amemfundisha kwa njia nyingine sasa. Alifunzwa na Roho Mtakatifu kumngojea Bwana, haidhuru shauku zake zilikuwa ni nini.

¹⁰⁰ Sasa nitaninii, kwa msaada wa Roho Mtakatifu, nitawaonyesha jambo fulani. Mnaona? Sasa hebu na tuchukue tu mfanu.

¹⁰¹ Siku moja, Paulo na Sila, wakishuka kuja barabarani katika mji fulani ambako walikuwa wakifanya uamsho. Na maskini msichana aliyepagawa na pepo alishikilia kumfuata, akipiga makelele nyuma yake. Na hapana shaka Paulo alijua ya kwamba alikuwa na mamlaka, kama mtume, kumkemea huyo pepo mchafu atoke ndani ya mwanamke huyo. Lakini je! mlitambua? Yeye alingojea, siku baada ya siku, mpaka, mara, Roho Mtakatifu akasema naye, kasema, “Ule wakati umewadia.”

¹⁰² Ndipo akasema, “Ewe pepo, toka ndani yake.” Unaona? Yeye alijua kumngojea Bwana.

¹⁰³ Na hapo ndipo mahali ambapo watu wengi siku hizi wanaleta fedheha juu ya Neno. Wanatoka wakiwa na lengo. Ni miamsho mingapi imeachwa ikiwa baridi kwa sababu ya jambo kama hilo, kwa sababu mwinjilisti huyo hangojei kuona yale Bwana anataka kusema! Baadhi yao wanasema, “Njoni hapa,” nao—nao wanaenda sasa hivi kwa sababu shi—shirika lilisema, “Nenda.” Na Roho Mtakatifu angesema jambo tofauti. Hata hivyo, lengo la mtu huyo kuwa mzee wa jimbo, ama—ama kitu kingine, ama mzee fulani, ama askofu fulani, ama kitu kingine kingimvuta. “Huna budi kwenda.” Na, hata hivyo, yeye anajua vizuri zaidi. Roho Mtakatifu akisema, “Nenda *hapa*.” Unaona? Yeye ametiwa nira kwa dhehebu lake. Yeye ni mfungwa wa dhehebu hilo.

¹⁰⁴ Lakini endapo amefungiwa nira kwa Kristo, yeye anaongozwa na Roho Mtakatifu. Yeye...?..Unaona? Yeye, yeye amefungwa nira, ni mfungwa. Haileti tofauti yoyote yale kitu chochote kingine kinasema; ni—ni—ni—ni shaba iliayo na upatu uvumao. Yeye husikia tu Sauti ya Mungu, naye hunena tu wakati inapotokea. Hasemi kitu.

¹⁰⁵ Mtu fulani anasema, “Loo, loo, Ndugu Jones!” Ndugu Roberts, ama wengineo, watu hawa mashuhuri nchini mwetu leo, kama Tommy Hicks, ama—ama—ama Oral Roberts, ama—ama

Ndugu Tommy Osborn, baadhi ya hao wainjilisti mashuhuri. Kama mtu fulani angesema, “Aisee, njoo huku, Tommy. Wewe ni mtu mashuhuri wa Mungu.” (Ama Oral.) “Nami—nami nina m—mjomba aliyelala hapa, ambaye—ambaye amefungwa kabisa. Naye—naye ni mgonjwa. Ninataka uje huku. Ninaamini una nguvu za kumponya.” Unaona?

Na labda Roho Mtakatifu angemwambia, “Si wakati huu.”

¹⁰⁶ Lakini, hata hivyo, kwa ajili ya urafiki wa mtu huyo, anawajibika kuambatana naye. Asipoenda, anakuwa adui wa mtu huyo. Mtu huyo anasema, “Vema, alienda kwa *nanii*, akamponya mtoto yule ama mvulana yule. Ninajua alimponya. Nami nimekuwa ni rafiki yake, kwa miaka kadhaa, unaona, wala asingekuja nyumbani kwangu.”

¹⁰⁷ Lakini kama ameshurutishwa na Roho Mtakatifu asiende, afadhali asiende, kama yeye amefungiwa nira pamoja na Mungu. Rafiki yake, yeye anampenda. Lakini ni afadhali aongozwe na Roho Mtakatifu kwenda kule, kwa sababu haitafaa kitu, haidhuru. Mimi ninapitia hilo mara nyingi sana.

¹⁰⁸ Lakini Paulo alingojea tu Roho amwambie la kufanya. “Mngojee Roho,” kasema. Yeye alisimama usiku mmoja, akihubiri. Kisha akatoka nje kule. Akamwona kilema. Na mara, Roho akanena naye, naye akasema, “Naona.” Vipi? Vile vile alivyoona watapata ajali, kwenye kisiwa. Unaona? “Naona ya kwamba una imani ya kuponywa. Simama kwa miguu yako. Yesu Kristo alikuponya.” Unaona? Haya basi. Yeye—yeye alikuwa. . . Alikuwa amefungiwa nira. Huenda alifanya uamsho wa juma moja kule wala hakuna kitu kilichokuwa kimetukia, bali hata hivyo alimngojea Roho Mtakatifu aseme. Unaona? Yeye alifungiwa nira kwa ombi hilo.

¹⁰⁹ Sasa unasema, “Ndugu Branham, unapinga yale uliyosema Jumapili, kuhusu wewe kuwa umekuwa ukingojea wakati huu wote.”

¹¹⁰ Na, ila, kumbukeni, Roho Mtakatifu ndiye aliyesema nami huko barabarani, na kusema, “Ninakutuma urudi miongoni mwa wagonjwa na wanaoteseka.” Unaona? Ni kumtii Roho Mtakatifu. Sikwenda mpaka aliponiambia niende. Nilikuwa nikingojea BWANA ASEMA HIVI, mpaka nikapata BWANA ASEMA HIVI. Sasa, hilo ni tofauti. Unaona? Sasa, Hilo, Hilo linaleta tofauti. Naam.

¹¹¹ Yeye alilingojea Neno la Bwana. Alisukumwa katika Roho, kufanya tu mapenzi ya Mungu, ndipo akawa mfungwa wa Yesu Kristo. Enyi marafiki, laiti tungaliweza tu kuwa wafungwa!

¹¹² Ninajua kuna joto. Lakini mimi—ningependa kutaja watu wengine wachache, mkiniruhusu. Nina kama sita ama wanane walioandikwa hapa chini. Lakini mimi—ningependa kumtaja mtu mwingine mmoja tu ama wawili.

113 Hebu tuchukue maisha ya Musa. Yeye alizaliwa mkombozi. Naye a—alijua jambo hilo, ya kwamba alizaliwa mkombozi.

114 Lakini kabla sijazungumza kumhusu Musa, ningetaka kutoa tamshi hili, ya kwamba, Mungu daima inabidi kumchukua mtu yeyote, ambaye atatumikia kwa uaminifu, kuwa mfungwa Wake. Mtu hana budi kusalimisha kila kusudi alilo nalo, kila kitu alichote yeye, kila—kila kitu, maisha yake, nafsi, mwili, mapenzi, matakwa, na kila kitu kingine, na kuwa kabisa mfungwa, kwa Kristo, ambaye ni Neno, kumtumikia Mungu.

115 Huenda ikakubidi kuenenda kinyume, katika maamuzi yako yaliyo bora. Labda, katika dhehebu fulani, huenda ukawazia ya kwamba wangekuinua na kukupa kitu fulani kikubwa, ambacho ungeweza kukitangaza. Bali unajikuta vipi? Unajikuta umeshindwa, baada ya kitambo kidogo, mpaka Mungu anapoweza kumpata mtu ambaye yuko tayari kuwa mfungwa Kwake.

116 Mungu anatafuta wafungwa. Daima amewatafuta. Unaweza ukatafuta kote katika Maandiko. Mtu hana budi kuwa mfungwa wa Kristo, dhidi ya chochote kile. Kwa hiyo, huwezi kuunganishwa na chochote ila Kristo; hata baba yako, mama yako, ndugu yako, dada yako, mume wako, mke wako, yeyote yule. Umeunganishwa tu na Kristo, na Yeye pekee, ndipo Mungu anaweza kukutumia. Mpaka wakati huo, huwezi.

117 Nikitoka nje, mara nyingine huwakemea watu. Mnaona? Ni—ninajaribu kuwafanya mjifungue. Huna budi kupata mahali pa kuanzia, kama vile wakati mwingine ninawakemea wanawake wanaokata nywele zao na kuvaa nguo hizi, na wanashikilia na kudumisha maungamo yao ya Ukristo. Wanasema, “Hilo ni jambo dogo.” Vema, huna budi kuanzia mahali fulani. Kwa hiyo anzia papo hapo, katika ABC zako. Unaona? Na uachane na kujifananisha na ulimwengu, kwa vyovyote vile, na uwe mfungwa wa Kristo. Na halafu usonge mbele tu, ukatilie mbali kila kitu, mpaka hatimaye mstari wa mwisho umekatiliwa mbali. Ndipo wewe ni—wewe ni. . . Wewe ni mfungwa basi. Unakuwa mkononi Mwake. Yeye, Yeye amekushika kwa mkono Wake.

118 Sasa, Musa alijua ya kwamba alizaliwa mkombozi. Alijua hilo. Na je! mlitambua, pamoja na lengo alilokuwa nalo Musa; akijua ya kwamba mama yake alikuwa amemwambia kule, kwa kuwa alikuwa ni yake wake.

119 Hapana shaka, huyo mtoto mdogo Musa alipozaliwa, kwamba mama yake alisema, “Unajua, Musa, wakati. . . Mimi na baba yako, Amramu, tuliomba sikuzote. Tulijua, na kuona katika Neno, wakati ulikuwa umewadia wa kuja kwa mkombozi. Nasi tuliomba, ‘Bwana Mungu, tunataka kumwona huyo mkombozi.’ Usiku mmoja, Bwana alitwambia, katika ono, ya kwamba wewe ungezaliwa, nawe ungekuwa ndiwe huyo

mkombozi. Hatukuogopa amri ya mfalme. Hatukujali aliyosema mfalme. Basi, tulijua ya kwamba wewe ulizaliwa mkombozi. Sasa, Musa, tulijua ya kwamba tusingeweza kukulea vizuri.”

¹²⁰ Sasa kumbukeni, walikuwa kule, miaka mia nne huko Misri. Mnaona?

¹²¹ “Na sisi—sisi tulitaka kukupa ki—kitu sahihi, elimu nzuri, mafunzo yanayofaa. Kwa hiyo, nilikuchukua na kukuweka katika kisanduku kidogo, na nikakuweka katika Nile. Na ni ajabu jinsi gani kwamba, mkondo ulikichukua kijisanduku hicho kupitia kwenye nyasi na matete, ukakileta moja kwa moja huku chini, maili kadhaa, na kukipeleka moja kwa moja kwenye ikulu ya Farao, ambapo nanii wake... Binti Farao alikuwa, mahali kidimbwi chake cha kuogelea kilipokuwa. Na jinsi ambavyo—ambavyo nilijua ya kwamba angehitaji mwanamke wa kukulea.”

¹²² Na katika siku hizo, kwa kweli, hawakuwa na chupa hizi za kunyonyeshea watoto, kwa hiyo ilimbidi awe na—na yaya aliyeajiriwa kumnyonyesha. Kwa hiyo... .

¹²³ “Na Miriamu, nikamtuma kule. Naye akasimama pale, naye akasema, ‘Ninajua mahali ninapoweza kumpata yaya wa kumnyonyesha,’ naye akaja akaniita. Na, Musa, milango yote imefungwa. Mpenzi, wewe una umri wa miaka kumi na sita sasa, nawe utakuwa mwana wa Farao. Na siku moja utakuwa mkombozi ambaye atawatoa watu hao huku.”

¹²⁴ Shauku za Musa zikaanza kukua. “Nitasoma, mama. Nitasoma kila kitu niwezacho. Unajua nitakalofanya? Nitajifunza jinsi ya kuwa mwanajeshi, nami nitajua jinsi ya kuwatoa hawa watu hapa. Nitakuwa jemadari mkuu, askofu, kwa hiyo nitajua jinsi ya kufanya jambo hilo. Nami nita—nitawatoa. Nitapata Ph.D yangu ama LL. Nitawatoa.”

¹²⁵ Kama vile “Baba Chiniquy,” kama umewahi kuvisoma vitabu vyake. Vema. Yeye “atawakomboa Waprotestanti wote,” mwajua, naye akawa mmoja, mwenyewe. Kwa hiyo, kasisi huyu mashuhuri, miaka kadhaa iliyopita, “Baba Chiniquy,” mnapaswa kupata kitabu chake na kukisoma. Wanamwita, “baba.” Yeye ni Ndugu Chiniquy tu, ndivyo ilivyokuwa. Hatumwiti mtu yeyote “baba,” namna hiyo. Kwa hiyo tunaona ya kwamba—ya kwamba sisi... Alikuwa anaenda kuisoma Biblia, kusudi aweze kutoka aende huko nje na kuikosoa dini ya Kiprotestanti na kuwafanya wote Wakatoliki. Na wakati alipoanza kuisoma Biblia, Roho Mtakatifu alimjilia, naye akampokea Roho Mtakatifu, na ndipo—ndipo akawa ni mmoja wao.

¹²⁶ Kwa hiyo basi angalia jambo hili, ya kwamba Musa alipata mafunzo yote. Kwa sababu, yeye—yeye alijua. Alikuwa mwerevu sana, amelimika sana, mwenye akili nyingi! Mpaka, hakuna mtu yeyote... Hata angeweza kuwafundisha Wamisri.

Mpaka, angeweza kuwafundisha wanasaikolojia wao. Angeweza kufundisha majemadari wao—wao kwamba nguvu za kijeshi zilikuwa ni nini. Alikuwa ni mtu mashuhuri. Nao watu walimwogopa Musa, kwa sababu ya ukuu wake. Loo, usomi wa jinsi hiyo! Jamani! Alikuwa ni askofu mkuu, ama labda kama papa. Alikuwa ni mtu mkuu. Naye alikuwa ni m—m—mtu mwenye nguvu. Naye alijua ya kwamba alizaliwa apate kufanya jambo hili, na alikuwa amefunzwa, akiwa na lengo kuu, kufanya hivyo.

¹²⁷ Ni kama tu ilivyo siku hizi. Sisemi ya kwamba watu, wakijifunza kwenye shule hizi, sisemi ya kwamba... Kama walivyo huku Magharibi sasa, watajenga shule ya theolojia ya dola milioni mia moja na hamsini, unaona, ya Kipentekoste, shule ya dola milioni mi—mia moja na hamsini. Kwangu mimi, hizo zinapaswa kupewa wamishenari hudumani. Unaona? Unaona? Unaona? Lakini, chochote kile, wanafanya nini wanapotoka humo? Wao ni nini? Kundi la mariki. Kweli kabisa. Na basi hivyo ndivyo wanavyotoka. Imekuwa hivyo daima, hao wengine, na huo ni mstari ule ule. Unaona?

¹²⁸ Sasa, tunaona, ya kwamba, wakati, Musa, katika mafunzo yake yote, na leo hii, pamoja na mafunzo yote, kuwafanya maaskofu wakubwa na kadhalika, lengo lile kubwa, la juu, tutafanya nini? Malengo yetu yanakuwa tu kama ya Musa yalivyokuwa. Unaona?

¹²⁹ Mungu, kabla hajamshika mtu huyo mkononi Mwake, ilimbidi kumvua lengo lake. Ilimbidi kumvua mafunzo yake yote.

¹³⁰ Alitoka akaenda, naye akawakomboa; alimwua Mmisri mmoja. Naye, na wakati alipofanya hivyo, alikuta kwamba alikuwa makosani. Asingeweza kufanya hivyo. Haikuwa hivyo. Ndipo ilimbidi Mungu kumpeleka huko nje nyikani, katika jangwa, mahali pa jangwa.

¹³¹ Unaona, kwa namna fulani ni ajabu, jinsi ambavyo hawa jamaa, ambao Mungu ana ujumbe kwa ajili yao. Yeye huwapeleka jangwani.

¹³² Alimpeleka Paulo jangwani, kumfunza, kumwambia kwamba ono hili lote kuu lilikuwa ni nini, huko jangwani. “Nenda kwenye jangwa fulani.” Naye akakaa huko mpaka Mungu akamjulisha kabisa la kufanya.

¹³³ Na wakati wa Musa, Yeye alimchukua akampeleka jangwani. Akamweka huko nje kwa muda wa miaka arobaini, akamvua theolojia yake yote na lengo lake lote. Loo, ni wakati wa jinsi gani, kwamba angeangalia nyuma na kuona kushindwa kwake. Na jinsi ambavyo sisi, usiku wa leo, tunapaswa kufanya jambo lile lile, tunapoona lengo letu.

134 Angalia uamsho wa uponyaji, na uone kama Bwana alifanya jambo fulani miaka michache iliyopita, kuanza kuurudisha uponyaji kwa wagonjwa, na kadhalika.

135 Kila mtu, kila dhehebu, ni kwa sababu Huo haukuja kwenye dhehebu lao, iliwabidi kujipatia mponyaji. Nasi tumefanya nini? Hebu na tuliangalie kwa dakika moja. Tumefanya jambo lile lile ambalo Musa alifanya. Tumetoka tukaenda na kujaribu sana kujibunia namna fulani ya muujiza. “Nilisikia harufu ya ugonjwa fulani. Ni—ni—nilikuwa na damu mkononi mwangu,” na kujibunia muujiza. Unaona? Nasi tumepata nini? Baadhi ya watu wameingia katika majaribio makali sana, hata wamevunjika moyo na wamekuwa walevi wa kawaida, wendawazimu, na wamerukwa na akili zao. Nao wakageuka na kurudi nyuma kabisa, utaratibu kutokana na malengo ya kipentekoste, wakarudi nyuma wakaunda madhehebu na kadhalika tena. Unaona?

136 Tumefanya nini? Tumeua kama Mmisri mmoja. Hiyo ni kweli. Nasi tumejaribu. Tumejikakamua. Tumelipia. Tumeshughulika, tukaenda usiku kucha katika mikutano ya maombi, mpaka tukapwelewa na sauti. Na—na kujaribu kujibunia kitu fulani, na kutia chumvi, na vitu hivi vyote vya namna hii, na tunaona ya kwamba tumeshindwa kabisa. Tunahitaji kurudi jangwani. Kweli. Naam, bwana. Majaribio na mapambano. Kwa nini tusijisalimishe tu? Hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya, unaona, kurudi na kujisalimisha. Mbona, tumefanya jambo lile lile walilofanya, jambo lile lile alilofanya Musa. Halifai kitu. Baada ya miaka arobaini, alijikuta ni mfungwa wa Neno la Mungu. Tunajaribu kufanya nini?

137 Wakati, ile Baraka kuu ilipotokea, na madhihirisho ya mambo haya yote makuu ambayo Mungu ametwambia juu yake: jinsi ambavyo hatuna budi kuzaliwa mara ya pili; na jinsi inavyotubidi kumpokea Roho Mtakatifu; ubatizo katika Jina la Yesu Kristo; na mambo haya yote hapa.

138 Unaona, watu, badala ya kukaa kwenye hilo Neno, kujifunga hatamu pamoja Nalo, wao wanafanya nini? Walianza na nadharia yao wenyewe ya kimadhehebu, ambayo tayari ilikuwa imeshindwa, na kujaribu kujibunia kitu fulani kionekane kama Kweli.

139 Afadhali nikatize moja kwa moja hapo. Unaona? Nina hakika ninyi mna hekima ya kutosha kujua kile ninachomaanisha. Mnaona? Lakini, mbona, angalia jinsi lilivyofanya. Wazia jambo hilo.

140 Tuna nini, usiku wa leo, ila ta—ta—taifa lililojaa watu wa kimadhehebu ambao wanayakana Maandiko ya Mungu; ambao wangeuita U—U—Uzima wa Roho Mtakatifu, kwamba, “Ulikuwa ni ku—kuwasiliana kimawazo,” ambao wangeukataza huo kuingizwa kanisani mwao. Wala wasingekuruhusu kutaja

Neno moja kuhusu uzao wa nyoka, usalama wa Milele, na mambo ambayo Roho Mtakatifu ameyafunua na kuthibitisha kwamba ni Neno. Nilitoa changamoto baada ya changamoto, waje wanithibitishie kwamba ni uongo.

¹⁴¹ Wamepata nini? Kitu kile kile ambacho Luther alikuwa nacho, hao wengine, unaona, alimuua Mmisri. Tunapaswa... Ilikuwa ni kitu gani? Labda alimfanya mtu fulani kuanza... kuacha kuiba, ama labda kuishi mwaminifu kwa mke wake. Lakini mlimfanya nini kutokana na hilo? Mfuasi wa kanisa. “Njoo ukajiunge na kundi letu.” Unaona?

¹⁴² Mtu huyo aliyekufa anayenuka ndicho kitu pekee angaliweza kukielekezea vidole vyake, kuonyesha mafanikio yake, ya miaka arobaini ya mafunzo; maskini Mmisri anayenuka amewekwa pale, ameoza na ni maiti.

¹⁴³ Hivyo ni karibu jinsi ilivyo usiku wa leo. Kitu pekee tunachoweza kukielekezea kidole, kwa uamsho ambao umevuka ng’ambo (unavyojiita), ni wafuasi wa kanisa wanaonuka ambao hawajui zaidi juu ya Mungu kuliko Mhotentoti anavyojua juu ya hekaya za Kimisri. Kweli. Hilo, ungewaambia juu ya Neno la Mungu, wanasema, “Siamini Hilo.” Wanasema, “Sijali unalosema, siliamini.” Unaona? Unaona? Hilo ni jambo baya sana kulazimika kulirejea, kwa majaribio yote magumu na mapambano na kila kitu tulicho nacho.

¹⁴⁴ Labda tungeelekeza kwenye shule kubwa, bali imekufa. Tungeweza kuelekeza kwenye dhehebu, bali limekufa. Linanuka. Ni kama tu kitu cha kwanza tulichotoka kwake. “Kama vile nguruwe akienda kwenye kugaagaa kwake, na mbwa kwenye matapiko yake,” tunaporudi. Mmisri mmoja aliyekufa.

¹⁴⁵ Hapana shaka ila mtu fulani alisema, “Musa, vema, hivi huwahurumii watu tena? Uliitiwa jambo hili.” Mtu fulani aliyemjua Musa, na aliyejua aliitwa kwa ajili ya jambo hilo. “Na huninii... Huwahurumii watu?”

“La, bwana.”

¹⁴⁶ “Vema, kwa nini hutoki nje, huku, ukifanya jambo *hili*? Na kwa nini huko hapa nje, ukijaribu jambo *hili*? Na kwa nini huambatani na hao wengine?”

¹⁴⁷ Musa alikuwa huko nje akivuliwa, mpaka akapata tukio penye kijiti kilichowaka moto, ambacho kililitangaza Neno. “MIMI NDIMI Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Nami ninakumbuka ahadi Yangu. Nami nimeshuka kuja kuwakomboa. Ninakutuma kuwakomboa.” Ndivyo ilivyokuwa.

¹⁴⁸ Aliliona Neno, sio lengo la watu ama shauku za watu. Ndipo akafanyika nini? Hakutaka kuwakabili Wamisri tena. Hakutaka kukabiliana na jambo hili tena. Bali akawa mfungwa. Amina. Miaka arobaini ya kutoroka, kuvuliwa, bali basi akawa mfungwa, kwenye kijiti kilichowaka moto, Musa mwenye nguvu

pamoja na akili zake zote. Biblia ikisema ya kwamba Musa alikuwa mtu mwenye nguvu katika neno ama katika tendo, huko Misri.

¹⁴⁹ Lakini angalia kile mwanatheolojia huyo mwenye nguvu alichofanya Mbele ya kijiti kilichowaka moto. Alikiri tu kushindwa kwake. Wakati alipoona kusudi halisi la Mungu, alikiri kuwa hakuwa na uwezo wa kufanya jambo hilo. Hata hivyo, alikuwa amefunzwa katika theolojia yote ambayo wangeweza kumpa, alifunzwa katika shule iliyo bora kabisa. Lakini, hata hivyo, angefanya nini wakati yeye... ile Nguzo ya Moto ikining'inia pale kichakani? Kasema, "Hata siwezi kuzungumza na Yeye. Bwana, mimi ni nani, hata niende?" Unaona?

¹⁵⁰ "Vua viatu vyako, Musa. Ninataka kuzungumza nawe. Jivue kabisa, hata viatu vyako. Uko—uko chini kabisa sakafuni tena. Ninataka kuzungumza nawe."

¹⁵¹ Asingeweza hata kuzungumza. Hatimaye, mfungwa aliyeteuliwa, nabii aliyeteuliwa, kama tu vile Paulo alivyokuwa ameteuliwa. Musa alikuwa ameteuliwa, mkombozi. Na halafu basi, hatimaye, Mungu alimfanya raia wake aliyeteuliwa mfungwa Wake. Loo, haleluya! Angeweza tu kusonga mbele jinsi Neno la Mungu lilimsogeza mbele. "Nitasema ni nani aliyenituma?"

"MIMI NIKO."

"Nitafanyaje?"

"Nitakuwa pamoja nawe."

¹⁵² "Naam, Bwana, kama tu usemavyo Wewe. Mimi hapa." Loo, jamani! Kwamba, yeye ni mfungwa.

¹⁵³ Anaenda kinyume na mawazo yake bora. Sasa, yeye alikuwa amefunzwa kuongoza jeshi. "Panga, juu! Geukeni!" Alifunzwa kwenda, "Magari, yote katika utaratibu! Mikuki, mbele! Shambulia!" Hivyo ndivyo atakavyoiteka. Hivyo ndivyo alikuwa amefunzwa.

Lakini akasema, "Nitatumia nini?"

Kasema, "Una nini mkononi mwako?"

¹⁵⁴ "Fimbo." Mungu hufanya mambo ya kuchekesha sana wakati mwingine, kwa akili ya kibinadamu. Unaona? Ana fimbo mkononi mwake. Masharubu yakining'inia chini. Umri wa miaka themanini. Mke wake juu ya nyumbu; mtoto ameketi nyongani mwake. Maskini, mikono dhaifu mikongwe ikining'inia chini; fimbo. Ni kichwa chake tu kilichosimama wima, kwa kuwa alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Kwa nini? Hatimaye alikuwa ametia nanga.

¹⁵⁵ Yeye alikuwa ni mfungwa. "Nitasogea tu wakati Neno litakaponisogeza. Nitana tu ambapo Neno linanena."

“Unaenda wapi?”

¹⁵⁶ “Nina agizo moja: kusimama mbele ya Farao na kumwonyesha, kwa fimbo hii, ya kwamba Mungu alinituma.” Amina.

“Utafanya nini baada ya hapo?”

“Yeye ataleta jambo litakalofuata, baada ya mimi kufanya hili.”

¹⁵⁷ “Haya basi. Una jambo moja tu la kufanya, hatua ya kwanza, usiku wa leo: jisalimishe, kuwa mfungwa. Usiwazie juu ya nafsi yako ama kitu kingine. Kuwa mfungwa.

¹⁵⁸ Musa alikuwa ni mfungwa, alikiri hata asingeweza kuzungumza. Hatimaye, wakati Mungu alipomshika mkononi Mwake, ambapo angeweza tu kusogea ambapo Mungu alimsogea. Ambapo, Yeye alimwambia Neno. Alijua lilikuwa ni Neno, ndipo akajisalimisha kwa Neno. Na Roho Mtakatifu pale, Mungu, alimfunga Musa hatamu kwa mapenzi ya Mungu.

¹⁵⁹ Hilo ni jambo lile lile alilomfanyia Paulo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye alimfunga Paulo hatamu; maskini Myahudi, mwenye pua iliyo chongoka, mwenye kejeli, loo, mwenye Ph.D. na ma-LL.D. yaliyoandikwa kote juu yake. Lakini Yeye alisema, “Nitamwonyesha mateso atakayopata kwa ajili ya Neno.” Unaona? Na yeye. . .

¹⁶⁰ Ndipo basi Paulo akiketi pale na akiona Neno, na akiona ya kwamba huyo alikuwa ni Yesu, ndipo akaiinua mikono yake na akafungiwa hatamu Kwake. Upendo wa Mungu ulimfunga hatamu kwa Neno. “Yeye atalichukua Jina Langu mbele ya Mataifa.” Huyoo akaenda.

¹⁶¹ “Musa, MIMI NDIMI Mungu wa baba zenu. MIMI NDIMI Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Ninakumbuka niliwaahidi, na wakati wa ahadi hiyo umekaribia. Nami ninayaona mateso ya watu Wangu. Ninaikumbuka ahadi Yangu. Nami nimeshuka kuja kukufunga hatamu. Unajua kile Neno lilichosema. Nimekufunga hatamu ushuke uende kule, nimekufunga hatamu kwa nguvu, ushuke uende kule na kuwakomboa watu Wangu. Basi chukua fimbo hiyo mkononi mwako, kama ushahidi, maana umeona mwujiza ukifanywa nayo.” Kama tu Daudi, akiwa na lile kombeo. Unaona?

¹⁶² Akafungwa hatamu, yeye mwenyewe, kisha akashuka akaenda. Hatimaye, Mungu alikuwa na mtu aliyekuwa chini ya mamlaka Yake, amefungiwa hatamu Kwake, wala asingesogea mpaka Neno la Mungu lilipomsogea. Laiti watu wanalifanya tu hivyo, siku hizi! Basi, yeye alikuwa ni mfungwa Wake, mfungwa wa upendo, amefungiwa nira katika kifungo cha upendo, pamoja—pamoja na Mungu, kama vile Paulo alivyokuwa amefungiwa nira kwa kifungo cha upendo kwa Mungu.

163 Ni kama tu Paulo, wote wawili walifunzwa kwa njia ile ile. Musa alifunzwa, mwajua, kuwakomboa wana wa Israeli kwa nguvu za kijeshi. Paulo alifunzwa kuwatoa kwenye mikono ya Warumi na kuwaweka huru, kwa nguvu zake kuu za kikanisa ulimwenguni siku hiyo. Shule kuu za kufundisha, alifunzwa chini ya Gamalieli.

164 Na wote wawili walienda jangwani; wakarudi wakiwa ni watu tofauti. Wote wawili waliiona ile Nguzo ya Moto. Na wote wawili walikuwa ni manabii. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wote wawili, manabii. Na wote wawili walizungumziwa na hiyo Nguzo ya Moto, kweli kabisa, ikija kwa ajili ya mkombozi. Hao hapo; walienda jangwani. Waliacha makazi yao wakaenda jangwani, wapate kujua. Waliwaacha watu wao na kila kitu, wapate kujua mapenzi ya Mungu. Unaona?

165 Walifunzwa katika njia moja; Mungu akawabadilisha kwa nyingine. Nao ilibidi kuwa mfungwa kabisa, wasije wakafanya jinsi walivyotaka kufanya, bali wafanye vile Mungu alivyowataka wafanye. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

166 Je! tuna dakika zingine kumi hapo, kufanya haya? [Ndugu Neville anasema, "Amina."—Mh.]

167 Nitamwendea mtu mwingine upesi sana. Ninaona mmoja mbebe zangu sasa. Jina lake ni Yusufu. Yeye alikuwa ni mwana aliyeteuliwa. Yeye alikuwa ni mfano mkamilifu wa Yesu Kristo. Alizaliwa nabii. Alikuwa ni nabii, pia. Unaona? Na sasa angeweza kuona ono. Na wakati akiwa bado ni mvulana mdogo, aliona ono la yeye mwenyewe ameketi kwenye kiti cha enzi, na ndugu zake wakimsujudia. Mnaona? Lakini angalieni. Yeye akawa. . . Alijisikia kana kwamba alikuwa ni jamaa mkubwa. Mnaona? Hao wote. . .

168 Lakini ilimlazimu Mungu kufanya nini? Alifanya jambo lile lile alilowafanyia hao wengine. Kwa sababu, Musa alikuwa ni mkombozi, Paulo alikuwa ni mkombozi, na sasa Yusufu alikuwa ni mkombozi. Yeye aliwaokoa watu wake kutokana na njaa.

169 Ilimbidi Mungu kumfanyia nini? Kumweka gerezani, kumweka moja kwa moja gerezani. Naam, bwana. Kumbukeni, yeye aliuzwa na ndugu zake, kwa Mmisri. Nao wakamuza kwa Potifa. Na Potifa akampa uhuru kidogo, na, muda si muda mnajua, huo uliondolewa kwake. Na hapo akaketi gerezani, akilia, akilia. Ilimbidi Mungu kumvua kila kitu.

170 Sasa angalia. Lakini, wakati wote, ninaamini, yeye, katika gereza hilo, aliweza kukumbuka ya kwamba ono lilisema ya kwamba ataketi kwenye kiti cha enzi, nao nduguze wangemsujudu, kwa maana yeye alijua ya kwamba karama yake ilitoka kwa Mungu. Naye alijua ilibidi lipate kutimia.

171 Laiti tungaliweza kuweka hilo moyoni mwetu, na kulingana na Neno la Mungu, kwamba katika siku hizi za mwisho

Yeye atakuwa na Kanisa, Yeye atakuwa na watu. Na mambo haya aliyohidi, Yeye atayafanya. Alisema atayafanya, nasi tunaishi katika wakati huo. Tumewasili. Yeye anajaribu tu kutufanya kuwa wafungwa halisi sasa, tumefungiwa ndani pamoja na Yeye.

¹⁷² Mlisikia ule wimbo wa kale mnaouimba, “Halafu nimefungiwa ndani pamoja na Mungu”? Ninataka kufungiwa ndani pamoja na Mungu. Sasa, hapo ndipo nilipowazia juu ya hili. Kufungiwa ndani pamoja na Mungu, hakuna lingine, nawe unasogea tu wakati Mungu anaposema usogee. Unatenda tu jinsi Mungu anavyosema utende, unaona, ndipo umefungiwa pamoja na Mungu.

¹⁷³ Sasa kumbukeni, yeye alikuwa akiwazia. Yeye pia alishindwa kabisa, kwa nafsi yake. Yote aliyoyajua, yote aliyoyafahamu, na kila kitu, alishindwa kabisa. Hayakufaa kitu. Aliwekwa chini ya hali ambayo hakuna mtu angalimsikiliza. Alikuwa ni mfungwa. Unaona? Aliwekwa katika hali, ambayo wasioamini wasingeweza kuamini. Mnaona ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Huduma yake ilikuwa ni bure. Watu waliangalia kwingine. Wasingemsikiliza huko gerezani. Huduma yake ingefaa nini? Angeweza kusimama kwenye nondo za gerezani na kuwahubiria; wangeendelea kushuka tu kwenda barabarani. Unaona? Lakini yeye akawa mfungwa. Na Mungu akamweka, mfungwa, mpaka gurudumu likafingirika vizuri. Kasema, “Huyu hapa mtu Wangu.” Utukufu! Kushindwa kukamilifu!

¹⁷⁴ Hatimaye, Mungu alimjia humo gerezani mwake. Kama vile Paulo, kama hao wengine wote, Yeye alimjia. Naye akatumia kipawa alichokuwa amempa, apate kumtoa humo. Hiyo ni kweli. Alimtoa kutoka gerezani mwake. Alifanya nini? Mara alipomtoa gerezani mwake, alipewa mamlaka na mfalme, mfalme wake, aliyeketi karibu naye, aliyekuwa chini yake. Alitolewa gerezani na kupewa mamlaka; mpaka, lolote alilosema, ilibidi litukie. Amina.

¹⁷⁵ Katika gereza lake, sikuzote alikumbuka, alizaliwa kwa kusudi fulani. Alikuwa ataketi karibu na mfalme. Hao wengine wote watampigia goti. Ono lake lilimwambia hivyo. Amina. Lakini kabla ya ono lake kuweza kutimia kikamilifu, alikuwa amekuwa mfungwa. Amina. Kisha akawa mtawala. Na wakati alipotoka gerezani mwake, na akawa mfungwa wa Neno la Mungu, hivi kwamba angesema tu yale Mungu aliyoweka kinywani mwake kusema, ndipo Mungu akatenda kazi kupitia kwake.

¹⁷⁶ Angalieni, ya kwamba Musa alikuwa na nguvu za kuwafunga wana wa Farao, alivyotaka. “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka.” Alikuwa na nguvu za kuwafunga wana wa Farao. Kama wao walikuwa ni mashemasi, ama wazee, ama walikuwa

wawakilishi wa nchi ama chochote walichokuwa. Yeye alisema, “Ninawafunga,” nao wakafungwa. Jambo lilikuwa ndilo hilo. Angeweza kufanya hivyo kwa neno lake mwenyewe, kwa mapenzi yake mwenyewe. Amina. Utukufu kwa Mungu!

Loo, nina kama tu dakika tatu zaidi, kwa hiyo ninatimiza neno langu.

177 Sasa tunaona, ya kwamba yeye—yeye alifanyika mfungwa kwa Mungu, kutoka kuwa mfungwa wa ulimwengu. Kutoka . . . Paulo, vivyo hivyo. Naye Musa, vivyo hivyo, kutoka kuwa mfungwa wa mawazo yake mwenyewe, akawa mfungwa wa Mungu. Ndipo wakati alipotoka, alikuwa na nguvu za Mungu. Na wakati alipofanyika Paulo . . . Wakati yale mawazo ya kale, ya Musa, aliyasalimisha na kuvuliwa hayo, alifanyika mfungwa wa Neno la Kristo. Angesogea tu popote . . .

“Unasema, ‘Ati Kristo?’”

178 “Alihesabu shutuma ya Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri.” Kwa hiyo yeye alikuwa ni mfungwa wa Kristo, kama tu Paulo alivyokuwa.

179 Kumbukeni, hao wote watatu walikuwa ni manabii. Unaona? Na ilibidi wavuliwe kabisa mawazo yao wenyewe, kusudi wafanyike wafungwa kwa mapenzi na njia za Mungu.

180 Halafu tunakumbuka, sasa, ya kwamba yeye alikuwa na nguvu za kufunga, kwa neno lake mwenyewe. Alikuwa na nguvu za kufungua, kwa neno lake mwenyewe. Angeweza kusema, “Ninakufungulia, katika jina la mfalme wangu.” Amina. Farao alimfanya Yusufu mwanawe.

181 Kristo anawafanya Wake, wafungwa wa upendo, Wanawe. Naye anawapa nguvu, kitu kile kile alichokuwa nacho. Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, unaona, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Hata zaidi ya hizi atazifanya.” Sasa mfungwa wa upendo wa Kristo anapewa mamlaka na Mfalme wake, ambaye ni Kristo. Amina. “Na amini nawaambia, mkiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ wala msitilie shaka moyoni mwenu; bali muamini mliyosema yatatimia, yatakuwa yenu. Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu; kama mmefungiwa nira Kwangu,” kwa maana Yeye na Neno Lake ni mmoja. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu. Huyu Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Yeye yule jana, leo, na hata milele! Mkikaa ndani Yangu,” si *hapa* na *pale*. “Kaeni ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu; ombeni mtakalo, ama msememe mtakalo, mtatendewa.” Yeye alikuwa na nguvu.

182 Angalieni, kabla hajatoka, ilibidi atolewe nje na kunyolewa. Mambo machache ilibidi yanyolewe kabla hajakutana na mfalme wake. Unaona?

¹⁸³ Loo, Mungu wakati mwingine huwatoa watu Wake nje jinsi hiyo, na kunyoa machache ya mapenzi yao wenyewe, anawaonyesha ya kwamba hawawezi kufanya tu walichotaka kufanya. Mnajua ninalomaanisha. Wao hawana—wao hawana uhuru wa kufanya yale wanayotaka kufanya. Kabla hawajayafikia mamlaka makamilifu na kuwa mtumwa wa upendo wa Kristo, hawana budi kunyolewa kisha watolewe. Wakati mwingine Yeye huwapeleka jangwani, kufanya hivyo, kuwanyoa kabisa. Kisha anawatoa, mtiwa mafuta, kutimiza kusudi ambalo Yeye amewachagulia wawe. Mnaona ninalomaanisha?

Ndugu, tuko katika wakati wa mwisho.

¹⁸⁴ Kumbukeni, nyakati zingine zote, yale Yeye aliyofanya. Daima imebidi kumchukua mtu na kumfanya mfungwa Wake, anaacha yote yaliyo yake. Ilimbidi kuacha kila kitu alichojua, asahau mafunzo yake yote, kila kitu, kusudi apate kujua mapenzi ya Mungu, na kumfuata Mungu.

¹⁸⁵ Hawezi kufuata chochote ambacho inabidi mwanadamu kufanya, na Mungu, wakati ule ule. Ni kinyume sana, kimoja kwa kingine. Huwezi kuwa unaenda Mashariki na Magharibi wakati ule ule. Huwezi kuwa unaenda kulia na kushoto wakati ule ule. Huwezi kuwa unafanya mema na mabaya wakati ule ule. Huwezi kuwa unamfuata Mungu na mwanadamu kwa wakati uo huo. La, bwana. Ama unamfuata Mungu au unamfuata mwanadamu.

¹⁸⁶ Sasa, basi, kama unamfuata Mungu na umejisalimisha kwa Mungu, basi unakuwa ni mfungwa kwa Mungu huyo, kwa Neno hilo, kwa mapenzi hayo. Haidhuru kitu kingine chochote kinasema nini, unakuwa m—mfungwa Kwake.

¹⁸⁷ Sikilizeni. Tuko katika wakati wa mwisho. Nami ningesema jambo hili kwa uchaji na heshima, wakati dakika chache za mwisho zinapopita. Angalieni. Kile Mungu, kwa maoni yangu, atakachofanya na hana budi kufanya, na atafanya katika siku hizi za mwisho, ni kupata chombo cha kuvunia. Hana budi kupata chombo, kupura sakafu. Mkulima yeyote, anapoenda kwenye mavuno yake, hana budi kuwa na chombo cha kuvunia; hakika, hana budi kuwa na mundu mkali ama chochote kile, chombo fulani, kupura nafaka. Na mavuno yameiva.

¹⁸⁸ Mungu, tuchukue mkononi Mwako. Tufanye watumishi wafungwa wa upendo Wako. Tutumie kama chombo, kuleta utambuzi kwa dunia hii yenye dhambi, iliyolaaniwa tunayoishi siku hizi, wa kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁸⁹ Kwangu mwenyewe, Mungu, jalia niwe mfungwa. Kama ndugu zangu wote wakinikataa, kama marafiki zangu wote wakinikataa, ninataka kuwa mfungwa wa Yesu Kristo na Neno Lake, nipate kufungiwa hatamu kwenye Neno Lake, kwa Roho

Mtakatifu, kumwona Roho Mtakatifu akilifanya Neno la Mungu kuthibitishwa na mambo yale yale aliyosema yangefanywa. Ninataka kuwa mfungwa wa Yesu Kristo.

Na tuombe.

¹⁹⁰ Sijui, usiku wa leo, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kama shauku hiyo tuliyo nayo, ya kuwa kitu kingine, ama labda ya jambo fulani ambalo huenda tukawazia, kuwa kitu cha kichoyo, sijui kama kwa namna fulani tusingeweza tu kuweka hilo kando.

¹⁹¹ Sijui kama mvulana mdogo hapa, usiku wa leo, ataangalia huku, aseme, “Nitakuwa, nitakapokuwa mtu mzima, nitakuwa kitu *fulani*.” Sijui kama ungeweza kuyahisi mapenzi ya Mungu yakitenda kazi maishani mwako, na kusema, “La, la. A-ha. Mimi—mimi. . . Shauku zangu zimepotea sasa. Kwa siku chache zilizopita, Roho Mtakatifu amekuwa akinena na mimi. Mimi—mimi—mimi—nataka kujitolea kwa Mungu, kuwa chombo cha kupuria kwa ajili ya siku hizi za mwisho.”

¹⁹² Msichana mdogo ambaye huenda akawa na shauku ya kuwa mama mzuri, ama—ama labda kuwa maskini binti mrembo, ama labda siku moja kuifanya Hollywood kuwa ndiyo kazi yako, si—sijui kama hutaki sasa kusalimisha shauku zako Mbele za Mungu na Neno Lake, kusikia wito wa Mungu maishani mwako mwenyewe. Mungu anajua kwamba wewe ni nani.

¹⁹³ Sijui kama kungekuwako na mhudumu karibu, ama mtumishi, mfanya kazi mahali fulani kanisani. Mimi huja tu hapa, mara moja moja. Mimi—sijui theluthi moja ya watu wanaoketi hapa, usiku wa leo, lakini mimi. . . kundi hili dogo lililo hapa. Sijui kama kungekuwako na mtu kama huyo, ambaye ungeweza radhi kusema, “Sijali yale asemayo mtu yeyote. Mimi ni mtumwa wa Mungu sasa. Mimi—mimi—nitahubiri Neno Lake, haidhuru. Sijali nini, dhehebu la—langu likinifukuza, ningali nitadumu na Neno hilo. Mimi—nitafanya hivyo. Mapenzi yangu ni mapenzi ya Mungu. Mapenzi ya Mungu ndiyo mapenzi yangu. Nitakuwa mfungwa wa Yesu Kristo. Kwa neema Yake na msaada Wake, nitafanya hivyo.”

¹⁹⁴ Wazieni jambo hilo, wakati tumeviinamisha vichwa vyetu. Ni wangapi walio na shauku hiyo, usiku wa leo? Naomba uinue mkono wako. Huo ni wangu, pia. Ninayasalimisha yote. Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, polepole sasa, wakati unapotafakari juu yake sasa, unapoomba.

Natoa yote,
Natoa yote
Yote Kwako, Mwokozi wangu mtakatifu,
Natoa yote.

Nato- . . .

¹⁹⁵ Kweli unamaanisha hilo? “Ninataka kuwa mfungwa. Mimi... Nichukue, Bwana. Nipeleke kwenye nyumba ya Mfinyanzi, usiku wa leo. Nivunjilie mbali, na unifinyange tena, hapa chini.”

Kwako, Mwokozi wangu mtakatifu,
Natoa yote.

¹⁹⁶ Baba wa Mbinguni, wakati wimbo ukiendelea kuimbwa, niliwazia inafaa sana wakati huu, ya kwamba ni—niukatize wimbo huo na kuzungumza na Wewe kwa dakika moja. Wakati watu wakiwaza, “Natoa yote,” Baba, jalia tufanye jambo hili, pamoja na kana kwamba hii ndiyo nafasi yetu ya mwisho kulifanya. Jalia tuje kwa uaminifu, tuje mezani pa Bwana, tuseme, tukiwa na mavazi yaliyooshwa, nafsi zilizooshwa, mapenzi yaliyooshwa, shauku zilizooshwa, kujitolea wenyewe.

¹⁹⁷ Na hebu Mungu na alichukue Neno Lake, akitufungia nira pamoja Nalo, Neno la Mungu. Pia jalia Roho Mtakatifu atuchukue sasa, tunapoisikia nira ikialika kuizunguka mioyo yetu. “Tangu usiku wa leo na kuendelea, ninakuchukua katika neno lako. Sasa usiwazie mawazo yako mwenyewe. Wazia mawazo Yangu. Wazia mapenzi Yangu. Nitakuongoza.” Mungu, jalia kwamba litakuwa ni tukio kwa kila mmoja wetu.

¹⁹⁸ Hawa vijana wanaoketi hapa; mume na mke; na wengine wakija kuwa mume na mke. Wapo wazee wanaoketi hapa, ambao ni wahudumu, wamekuwa barabarani. Na, Bwana, huyu hapa Ndugu Neville, mimi, ninakaribia huko juu kabisa kwenye ngazi. Siku zetu zinahesabiwa sasa. Hatua zetu zinapigwa kwa uangalifu zaidi kuliko vile tulivyozipiga. Tunaangalia mahali tunapokanyaga. Sisi si wepesi wa kutembea, tukinena kimwili, kama tulivyokuwa wakati mmoja. Lakini, Bwana, tunapoyaona maisha hayo ya kibinadamu yakitoweka, wala hakuna hatua yetu iliyo na hakika bila Wewe kuushika mkono wetu.

¹⁹⁹ Sasa, Mungu, tuchukue, je! utatuchukua? Ichukue mioyo yetu na mapenzi yetu mkononi Mwako, na jalia tuwe wafungwa, usiku wa leo, kwa Neno, kwa Kristo. Jalia tuishi maisha ya kitauwa hapa. Jalia wanawake hawa, vijana hawa wa kike, vijana hawa wa kiume, wavulana kwa wasichana, wayatoo maisha yao, Bwana. Na jalia shauku yao iwe ni shauku ya kumtumikia Yesu Kristo. Pia jalia tuwe mfungwa wa neema na mapenzi Yake ya Kiungu. Tujalie, Bwana.

²⁰⁰ Ndiyo yote nijuayo kufanya, Bwana. Maskini maneno haya yaliyovunjika-vunjika, na mimi—mimi ninatumaini ya kwamba utayaweka pamoja, vizuri. Maana, kuna joto hapa ndani, na watu wanataka kusikiliza, bali kuna joto sana. Na wengi inawabidi kwenda nyumbani na kwenda kazini mapema. Lakini jalia hizo mbegu zikae tu moyoni mwao, “mfungwa.”

²⁰¹ Waende nyumbani na kumwambia mke, wanaponinii... kabla hawajajiandaa kushuka kwenda na kuomba, alasiri ya

leo, ama jioni ya leo, kando ya kitanda, waangaliane, waseme, “Mpenzi, vipi kuhusu jambo hilo, usiku wa leo? Hivi kweli tumekuwa wafungwa wa Kristo na mapenzi Yake, ama—ama je! tunafanya kazi kwa mapenzi yetu wenyewe?”

²⁰² Jalia vijana wanaume na wanawake, kila mahali, hasa sana wale waliousikia Ujumbe, usiku wa leo, wajiulize wenyewe swali lilo hilo, “Je! niko tayari kuwa mfungwa, kuyaacha maisha yangu?”

²⁰³ “Yeye ayaokoaye maisha yake atayapoteza, bali yeye atakayeyapoteza maisha Yake kwa ajili Yangu atayapata.” Baba, tunajua, hiyo ni: kuwa mfungwa Wako, tupoteze malengo yetu wenyewe na shauku zetu wenyewe, tukapate Yako, ndipo tuna Uzima wa Milele. Tujalie, Bwana.

²⁰⁴ Jambo pekee nijualo, ni kuukabidhi sasa mkononi Mwako. Na jalia uzae matunda na kuleta vyombo vi—vikuu kwa ajili ya mavuno ya siku za mwisho, wanaume na wanawake, wavulana kwa wasichana, wajitolee kwa mapenzi makamilifu ya Mungu, na wawe wafungwa wa Yesu Kristo, kwa upendo Wake, wamefunganishwa kwa vifungo vya upendo wa Kiungu kwa Kristo. Tunaomba katika Jina Lake.

Natoa yote,

Na tusimame.

Natoa yote,

Yote Kwako, . . . ? . . . wangu

²⁰⁵ Hebu na tuseme tu hilo tena, huku macho yetu yamefumbwa na mikono yetu imeinuliwa.

Natoa yote,

Natoa yote

Yote Kwako, Mwokozi wangu mtakatifu,

Natoa yote.

²⁰⁶ Sasa, kama tutaviinamisha vichwa vyetu, na kabla ya wimbo wa kuwaruhusu mwondoke haujaimbwa, wa *Peleka Jina la Yesu*, nitaomba ya kwamba—ya kwamba ndugu huyu hapa . . . Ninasahau jina lake. Yule dada ambaye alishuhudia juu ya ono la giza linalokuja, ambaye aliponywa. Pia kumbukeni, alipoangalia tena, utaji huo ulikuwa umetoweka. Imani yake ilifanya hivyo. Turuhusu tuondoke kwa maombi, sivyo, ndugu? Na utuombee baraka za Mungu.



MFUNGWA SWA63-0717

(A Prisoner)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 17 Julai, 1963, kwenye Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org